# Sauti ya Sheria

Toleo Na. 1 — Julai - Desemba, 2025

Jarida

## Mafanikio katika Sekta ya Sheria, Usimamizi wa Mikataba na Uendeshaji Mashauri ya Madai na Jinai



**Mhe. Hamza S. Johari**
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

ISBN-13: 978-2820268600

# Yaliyomo

01 Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

02 Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

04 Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

05 Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

07 Majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

08 Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

10 Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Asisitiza Maslahi ya Taifa Kuendelea Kuzingatiwa kwenye Mikataba

12 OWMS Kuendeleza Uhusiano na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

14 Tumieni Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao Ipasavyo

16 Uzinduzi na Utiaji Saini wa Sheria Zilizofanyiwa Urekebu Toleo la Mwaka 2023

18 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yafanikiwa Kuokoa Zaidi ya Shilingi Trilioni 3.6

20 Viongozi, Wadau wa Haki Jinai Watembelea Magereza ya Keko, Segerea na Ukonga

22 Tunataka kuwa Champion wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050

24 Wakili Mkuu wa Serikali Awafunda Mawakili Kuhusu Uendeshaji wa Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

26 Kuweni Mfano wa Kusimamia Haki - Mkurugenzi Mwakitalu

28 Mabadiliko ya Sekta ya Sheria: Nguzo Muhimu ya Dira ya Maendeleo 2050

30 Wakili Mkuu wa Serikali Akutana na Mkurugenzi wa Benki ya Dunia

31 Jaji Mkuu Apongeza Taasisi Zinazounda Utatu kwa Kupunguza Msongamano wa Mahabusu Magereza

32 Mwanasheria Mkuu wa Serikali Anavyosimamia Upatikanaji wa Haki, Utekelezaji Dira 2050

36 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yawasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria

38 "Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni Jeshi la Kulinda Nchi Dhidi ya Uhalifu Wowote, Ndani na Nje ya Mipaka ya Nchi" - Dkt. Ndumbaro

40 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na "Curtis Law Firm" Kushirikiana Kuwajengea Uwezo Mawakili

41 Wananchi Watakiwa Kupata Elimu ya Mpiga Kura Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

43 Mafanikio ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita

45 "Kitu cha Kwanza kwa Mwanasheria ni Kuhakikisha kila Jambo Analifanya kwa Wakati na Ubora" - Mwanasheria Mkuu wa Serikali

47 Mahakama ya EAC Yatupilia Mbali Pingamizi la Bomba la Mafuta Uganda - Tanga

49 Mashirikiano Kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na UNODC Yazidi Kuimarika Katika Kutokomeza Kesi za Ukatili wa Kijinsia

51 Kamati ya Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo Yazinduliwa Singida

53 Mahakama Yatoa Uamuzi Kuhusu Uhalali wa Uwepo wa Pori la Akiba Pololeti, Wilaya ya Ngorongoro, Arusha

55 DPP Akabidhiwa Juzuu za Toleo la Urekebu wa Sheria la Mwaka 2023

56 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kuboresha Sheria Kuelekea Utekelezaji wa Dira 2050

58 Rufaa Inayopinga Ujenzi wa Bomba la Mafuta Yatupiliwa Mbali

60 Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Azitaka Kamati za Ujenzi Wilayani Kusimamia Kikamilifu Miradi ya Ujenzi

61 Watumishi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Wakumbushwa Kuendelea Kufanya Kazi kwa Ufanisi

63 Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Awaongoza Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kushiriki Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake

64 "Uchunguzi wa Makosa ya Kifedha ni Nguzo Muhimu Sana Katika Mapambano Dhidi ya Uhalifu wa Kiuchumi" - Mhe. Rose Ibrahimu

65 “Sisi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tunaamini Nyinyi Wahariri ni Askari wa Kalamu” - Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

67 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yasogeza Huduma Karibu na Wananchi

68 Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Washiriki Kwenye Maadhimisho ya Mei Mosi 2025 Mkoani Singida

69 Bunge Lapitisha Miswada Miwili ya Marekebisho ya Sheria

70 “Toeni Elimu ya Sheria za Uchaguzi kwa Wananchi” - Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

71 Kamati ya Bunge Yapongeza Serikali Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Temeke



**Leila Muhaji**
**Mhariri**
*Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali*



**Prisca Ulomi**
**Mhariri**
*Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali*



**Rebecca Kwandu**
**Mhariri**
*Ofisi ya Taifa ya Mashtaka*

# Tahariri ya Wahariri

Karibuni ndugu wasomaji katika Jarida hili la kwanza la pamoja lililosheheni maudhui ya Ofisi tatu ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Ofisi hizi tatu zinashirikiana katika kutoa huduma za kisheria kwa Serikali, Taasisi zake na wananchi kwa ujumla. Pamoja na majukumu ambayo yamekasimiwa kwa Ofisi hizi, vile vile zimekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Sekta ya Sheria inaimarika zaidi kwa kushirikiana katika kuhakikisha muendelezo wa mnyororo wa haki, amani na usalama kwa nchi na raia wake unapatikana. Jarida hili linaangazia masuala mbalimbali yaliyotekelezwa na Ofisi hizi tatu kwa lengo la kuhabarisha, kujenga uelewa na kuwafahamisha wasomaji na wadau masuala mbalimbali kuhusiana na Ofisi hizi.

Ofisi hizi tatu zimeundwa kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais ya Maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 48 la Mwaka 2018 ambapo Serikali ilifanya mabadiliko kwa OWMS na kuanzisha Ofisi nyingine mbili ambazo ni Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Baada ya maboresho hayo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikasimiwa majukumu ya kuishauri Serikali juu ya masuala yote ya kisheria ikiwemo Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania ni sehemu ya Mkataba ama ina maslahi katika Mikataba hiyo; kutoa ushauri kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Taasisi za Serikali kuhusu mchakato wa utungwaji wa sheria na masuala mengine yahusuyo sheria; kutoa ushauri stahiki wa sheria zilizotungwa na Bunge, Sheria Ndogo na maazimio mbalimbali; kuandaa miswada ya sheria kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni; kuandaa Hati zote za kisheria na Maazimio kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kupitia tangazo la Serikali Na. 50 la mwaka 2018, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa Serikali katika kuratibu, kusimamia, kushauri na kuendesha kwa ufanisi na ubora mashauri yote ya madai ikiwemo mashauri ya Haki za Binadamu, Katiba, Uchaguzi na Mashauri ya Usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali/taasisi zake au yanayofunguliwa dhidi ya Serikali/ Taasisi zake ndani na nje ya nchi. Lengo mahususi la kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwa ni kuimarisha huduma ya uwakili kwa Serikali na taasisi zake ikiwa ni pamoja na kujenga taasisi yenye uwezo wa kitaalamu ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Vile vile, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kupitia tangazo la Serikali Na. 49 imepewa jukumu la kusimamia haki jinai ikiwemo kufungua na kuendesha mashtaka ya umma mahakamani (isipokuwa mahakama za kijeshi) pamoja na kuratibu upelelezi katika vyombo chunguzi pamoja na kukagua Magereza na vituo vya Polisi; kusimamia kazi za Jukwaa la Haki Jinai la Taifa, Mikoa na Wilaya; kutoa ushauri wa kisheria kwa mamlaka mbalimbali katika masuala ya jinai; kuendesha na kusimamia kesi zinazohusu utaifishwaji wa mali na uhalifu; kutoa miongozo mbalimbali kwa wadau wa Haki Jinai kuhusu upelelezi na uendeshaji wa mashtaka; kuratibu mashauri yanayohusiana na uhamishwaji wa wahalifu kutoka ndani na nje ya nchi na kusaidia mamlaka za ndani na nje katika masuala ya Jinai na kushiriki kwenye utafiti wa kifo (inquests).

Hivyo, majukumu ya Ofisi tatu tajwa hapo juu ni Ushahidi tosha wa azma ya Serikali ya kuboresha Sekta ya Sheria nchini kwa kuunda Ofisi hizo ili kuweza kuongeza tija na ufanisi katika kuhudumia wananchi kwenye mnyororo wa upatikanaji wa haki; ulinzi na usalama wa raia na rasilimali za nchi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama; wadau na wananchi kwa ujumla.

Uwepo wa Ofisi hizi tatu na utendaji kazi wake umekuwa chachu kwa wataalamu wa Sekta ya Sheria nchini ambapo maboresho mbali mbali yameendelea kufanyika katika nyanja ya haki jinai na haki madai na kuwawezesha watendaji na wanufaika kuhakikisha uwepo wa mnyororo wa haki nchini.

Hivyo, Jarida hili la pamoja la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni jukwaa la kuwaleta pamoja wasomaji, wadau na wananchi kufahamu namna Ofisi hizi zinavyotekeleza majukumu yake ipasavyo.

Tunatoa rai kwa wasomaji wetu kutoa maoni, ushauri na mapendekezo ya kuboresha Jarida hili na utendaji kazi wa Ofisi hizi tatu kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla. Tunawatakia usomaji mwema. Karibuni.

# Majukumu ya
# Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni zao la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Majukumu ya Ofisi hii yanaelezwa katika Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, na pia Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa mwaka 2018 pamoja na Tangazo la Serikali Namba 48 la mwaka 2018.

Aidha, Kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais ya Maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 48 la Mwaka 2018, Ofisi hii inatekeleza majukumu yafuatayo;

### 1. Ushauri wa Kisheria

- Kuratibu Usimamizi wa Maafisa Sheria, Mawakili wa Serikali, na Wafanyakazi wengine wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara, Taasisi za Serikali, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- Kutunza na kuhuisha kanzi data ya Maafisa wa Sheria, Mawakili wa Serikali na Waajiriwa wengine katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara, Taasisi za Serikali, Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kushauri ipasavyo.

- Kutoa Ushauri kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakala, Wananchi, Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali juu ya masuala yote yanayohusu Sheria.

### 2. Upekuzi wa Mikataba

- Kuandaa na kutoa Ushauri wa Kisheria kuhusiana na Mikataba, Hati za Makubaliano na masuala mengine ya Kimkataba yanayoihusu Serikali;

- Kuhakiki, Kuratibu na Kutoa Ushauri wa Kisheria kwa Serikali kuhusiana na Mikataba ya Kikanda na Makubaliano baina ya Nchi na Nchi na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa inayohusisha Serikali;

- Kutoa Ushauri wa Kisheria kwa Serikali kuhusiana na Majadiliano katika Mikataba inayohusisha Serikali;

- Kufanya Utafiti kuhusiana na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa inayotaka Kuridhiwa/Kuingiwa na Serikali;

- Kutoa Ushauri wa Kisheria kwa Wizara, Serikali za Mitaa, Idara za Serikali na taasisi nyingine za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusiana na Mikataba, Hati za Makubaliano na masuala mengine ya Kimkataba yanayoihusu Serikali

### 3. Uandishi wa Sheria

- Uandishi wa Miswada yote ya Sheria ya Serikali;
- Kushauri katika masuala yote yanayohusiana na mchakato wa Utungaji wa Sheria;
- Kuandaa/Kuhakiki Sheria Ndogo zote Zinazotungwa na Wizara na Mamlaka nyingine;
- Kuandaa Maazimio kwa ajili ya Bunge kuridhia Mikataba na Itifaki za Kimataifa;
- Kufanya Urekebu wa Sheria Kuu na Sheria Ndogo zote kwa Kuzingatia Matakwa ya Sheria ya Urekebu wa Sheria, Sura ya 4;
- Kufanya Ufasiri wa Sheria Kuu, Sheria Ndogo na Nyaraka nyingine za Kisheria kwa kuzingatia Masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1; na;
- Kusimamia Utangazaji wa Miswada, Sheria Kuu na Sheria Ndogo zote katika Gazeti la Serikali

# Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali



**Mhe. Hamza S. Johari**

Mwanasheria Mkuu wa Serikali



**Samwel M. Maneno**

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali



**Neema Ringo**

Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Huduma za Ushauri wa Kisheria



**Sia B. Mrema**

Mkurugenzi wa Divisheni ya Mikataba na Makubaliano



**Buji E. Bampebuye**

Mkurugenzi wa Divisheni ya Mipango



**Faith Minani**

Mkurugenzi wa Divisheni ya Utawala na Rasilimali Watu



**Regina Mutagulwa**

Mkuu wa Kitengo cha Uhasibu na Fedha



**Felefu D. Magaka**

Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani



**Proscovia Ichwekeleza**

Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi



**Leila O. Muhaji**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini



**Emmanuel Chanya**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA



**Sunday M. Hyera**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Mikataba ya Kimataifa



**Mukabatunzi D. Rwakilomba**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha, Rasilimali na Uwekezaji



**Edson F. Mweyunge**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Manunuzi



**Ipyana A. Mlilo**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Uratibu



**Sylivia N. Matiku**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Huduma za Ushauri



**Elias F. Kissamo**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Majadiliano na Usimamizi wa Mikataba

# Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

## Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ina majukumu yafuatayo;

### Usimamizi na Uendeshaji wa Mashtaka

i.Kufanya uamuzi wa kufungua au kutofungua mashtaka;

ii.Kusimamia uendeshaji wa mashtaka yote ya jinai nchini isipokuwa yale yaliyo katika Mahakama za Kijeshi;

iii.Kusitisha kesi iliyofunguliwa mahakamani na mtu au mamlaka yoyote kwa kuzingatia matakwa ya sheria;

iv.Kuchukua na kuendesha mashtaka yaliyofunguliwa mahakamani na mtu au mamlaka yoyote kwa kuzingatia matakwa ya sheria;

v.Kukata rufaa au kufungua maombi au kujibu rufaa au maombi kwa niaba ya Jamhuri;

vi.Kuendesha na kusimamia kesi zinazohusiana na utaifishwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu;

### Kuratibu na Kusimamia Upelelezi

i.Kusimamia na kuratibu shughuli za upelelezi zinazofanywa na vyombo vya upelelezi/chunguzi;

ii.Kuagiza chombo chochote kinachohusika na upelelezi wa makosa ya jinai kuendesha upelelezi kuhusiana na taarifa zenye mwelekeo wa jinai zilizofika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

iii.Kukagua magereza na mahali popote wanapohifadhiwa wahalifu kwa mujibu wa sheria;

iv.Kusimamia kazi za Jukwaa la Haki Jinai la Taifa, Mikoa na Wilaya ;

v.Kuunda kikosi kazi kwa ajili ya kuchunguza na kupeleleza suala mahsusi la kijinai kadri atavyoona inafaa.

vi.Kutoa miongozo mbalimbali kwa wadau wa Haki Jinai kuhusu upelelezi na uendeshaji wa mashtaka;

vii.Kuelekeza na kushiriki kwenye utafiti wa kifo (inquests); na

### Usimamizi wa Jukwaa la Haki Jinai

i.Kusimamia kazi za Jukwaa la Haki Jinai la Taifa;

ii.Kusimamia kazi za Jukwaa la Haki Jinai la Mikoa;

iii.Kusimamia kazi za Jukwaa la Haki Jinai la Wilaya;

### Ushirikiano wa Kikanda

i.Kuratibu mashauri yanayohusiana na uhamishwaji wa wahalifu kutoka ndani na nje ya nchi;

ii.Kusaidia mamlaka za ndani na nje katika masuala ya Jinai ikiwemo kukusanya ushahidi;
Ushauri wa Kisheria

i.Kutoa ushauri wa kisheria kwa Mamlaka mbalimbali katika masuala ya Jinai;

ii.Kusimamia Maafisa, Mawakili wa Serikali na Maafisa wengine walioajiriwa au walioteuliwa kutekeleza majukumu ya kuendesha mashtaka.

# Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka



**Sylvester A. Mwakitalu**

Mkurugenzi wa Mashtaka



**Bibiana Joseph Kileo**

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka




**SIMON V. NTOBBI**

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu



**Javelin Rugaihuruza**

Mkurugenzi Divisheni ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi



**Mussa Magunguli**

Mkurugenzi Idara ya Mipango



**Faraja Nchimbi**

Mkurugenzi Divisheni ya Utaifishaji Mali, Makosa yanayovuka Mipaka



**Saraji Iboru**

Mkurugenzi Divisheni ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi



**Pendo Makondo**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka



**Zakaria Ndaskoi**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa ya Rushwa



**Materus Marandu**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Kudhibiti Mashtaka



**Agness Hyera**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utaifishaji na Urejeshaji Mali



**Seth Mkemwa**

Mkurugenzi msaidizi sehemu ya makosa ya udanganyifu na utakatishaji mali



**Bihaga Yogwa**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Rasilimali Watu



**Basilius Namkambe**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa yanayovuka Mipaka na Kupangwa



**Janethreza Kitaly**

Mkurugenzi msaidizi sehemu ya Usimamizi wa Kesi



**Lilian Nyenza**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Maktaba



**Agness Mtindi**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masijala ya sheria



**Frank Shame**

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA



**CPA Iddy Mboweto**

Mkaguzi Mkuu wa Ndani



**Rebecca Kwandu**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini



**Leonard Mehta**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya utawala



**Oswald Kyamani**

Mkurugenzi msaidizi sehemu ya Bajeti na Mipango



**Yohana Ngao**

Mkurugenzi msaidizi sehemu ya ufuatiliaji na tathimini



**Renatus Mkude**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa dhidi ya Binadamu na Utenga



**Salimu Msemo**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa ya Mazingira na Maliasili



**Monica Mbogo**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa ya Kimtandao



**Christopher Msigwa**

Kaimu Mkurugenzi Divisheni ya Makosa ya Udanganyifu, utakatishaj

# Majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Kwa mujibu wa Muundo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ina viongozi wakuu wawili ambao ni Wakili Mkuu wa Serikali ambaye ni mkuu wa taasisi na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ni Msaidizi Mkuu wa Wakili Mkuu wa Serikali na Afisa Masuhuli ambaye anawajibika kusimamia majukumu ya kila siku ya taasisi na mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wote waliopo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Yafuatayo ni majukumu ya Wakili Mkuu wa Serikali:-

1. Kuratibu, Kusimamia na Kuendesha mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali/Taasisi zake au dhidi ya Serikali/ Taasisi zake ndani na nje ya Nchi. Taasisi ni pamoja na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mamlaka na Mashirika ya Umma na pia Kuingilia kati (intervene) na Kuendesha mashauri yanayozihusu taasisi binafsi ambapo Serikali ina maslahi au kugusa mali za Umma,
2. Kuishauri Serikali kwenye mambo yote yanayohusu mashauri ya Madai na usuluhishi kwa weledi;
3. Kuandaa, Kufungua na Kuitetea Serikali na Taasisi zake katika Mahakama na Mabaraza ya ndani na nje ya Nchi zikiwemo Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Mahakama na Mabaraza ya Nchi za Nje na Mabaraza ya kimataifa.
4. Kusimamia na Kuratibu mwenendo wa mashauri yote ya Madai na usuluhishi yanayoihusu Serikali ambayo yapo Mahakamani na kwenye Mabaraza ya ndani na nje ya Tanzania ili kuhakikisha Serikali Inapata uwakilishi stahiki, kwa weledi mkubwa na wenye viwango;
5. Kusimamia na Kutoa Miongozo kwa Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali ambao wanahusika katika Uendeshaji wa mashauri ya Madai yanayoihusu Serikali;
6. Kusimamia na Kuratibu mashauri yote ya Madai na ya Usuluhishi yanayoihusu Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Idara mbalimbali na Mashirika ya Umma yaliyo katika Mahakama na Mabaraza;
7. Kuingilia kati na Kuchukua hatua Stahiki kwenye mashauri ya Madai yote yaliyo katika Mahakama yoyote ambayo yana maslahi ya umma;
8. Kutoa Maelekezo juu ya suala lolote kwa Afisa yeyote wa umma kwa ajili ya Kuwezesha usimamizi mzuri wa Mashauri yote ya Madal;
9. Kuhakiki na Kupata idadi ya Mashauri yote ya Madai yanayoihusu Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma na kuzipatia ufumbuzi;
10. Kufanya tafiti Mbalimbali za Kisheria ili kuhakikisha Serikali inapata uwakilishi na utetezi wenye hadhi ya juu pale inapokuwa na Mashauri Mahakamani ndani na nje ya Nchi;
11. Kutambua mashauri mbalimbali ya Madai yasiyo na tija na yanayoweza kuongeza hasara kwa Serikali na k uyatatua kwa njia za majadiliano na maridhiano nje ya Mahakama;
12. Kufanya Tathmini ya kina ili kubaini chanzo cha mashauri ya Madai yanayoihusu Serikali na namna ya kuyashughulikia kwa ufanisi;
13. Kuweka Utaratibu mzuri utakaowezesha Wizara, Idara na Taasisi za Umma, Kutunza na Kutoa taarifa/ kumbukumbu za Mashauri ya Madai yanayosimamiwa katika Wizara, Idara na Taasisi husika ya Umma;
14. Kufanya vikao mbalimbali na Wadau juu ya mashauri yasiyo na tija kwa Serikali na kuangalia ni kwa jinsi gani yanaweza kumalizika nje ya Mahakama na hivyo kuipunguzia Serikali gharama; na
15. Kuandaa Taarifa za Mashauri inayoendesha na Kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria.

# Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



**Dkt. Ally Possi**
Wakili Mkuu wa Serikali



**Alice E. Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali



**Mark Mulwambo**

Mkurugenzi wa Idara ya Madai



**Saddy Sevingi**

Kaimu Mkurugenzi - Idara ya Usuluhishi



**Camilius Ruhinda**

Kaimu Mkurugenzi - Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora



**Asha Hayeshi**

Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu



**Theresia Mpangala**

Kaimu Mkurugenzi - Idara ya Mipango



**Devota Ngulugulu**

Mhasibu Mkuu



**Joan John**

Mkaguzi Mkuu wa Ndani



**Prisca Ulomi**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini



**Hellen Lubogo**

Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi



**Aziz Makaburi**

Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia, Habari na Mawasiliano



**Kiuye Shemakame**

Kaimu Mkuu wa Kitengo
cha Huduma za Maktaba
na Utafiti



**Dennice Leonard**

Kaimu Mkuu wa Kitengo
cha Masijala ya Sheria



**Deodatus Nyoni**

Mkurugenzi Msaidizi -
Madai ya Ndani



**Vivian Ishengoma**

Mkurugenzi Msaidizi -
Katiba, Haki za Binadamu,
na Uchaguzi.



**David Zacharia**

Mkurugenzi Msaidizi -
Usuluhishi wa Ndani



**Mercy Kyamba**

Mkurugenzi Msaidizi
Udhibiti Ubora

Mkurugenzi Msaidizi
Usuluhishi wa Nje

Mkurugenzi Msaidizi
Madai ya Kimataifa

Mkurugenzi Msaidizi
Usimamizi wa Mashauiri




# Rais Samia Asisitiza Maslahi ya Taifa Kuendelea Kuzingatiwa kwenye Mikataba

*Na Leila Muhaji*

## Mikataba 1,799 ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na Hati 352 za Makubaliano zafanyiwa Upekuzi - Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inaendelea kuzingatia maslahi ya nchi kwenye Mikataba mbalimbali, ambayo nchi inakusudia kuingia, kwakuwa Kikatiba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo yenye dhamana ya Upekuzi na Tathmini ya Mikataba inayoingiwa na Serikali na Taasisi zake.

Mhe. Rais aliyasema hayo tarehe 03 Februari, 2025, wakati alipokuwa Mgeni rasmi katika Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Sheria nchini, yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini, Dodoma.

Aidha, Dkt. Samia aliwataka Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kuzingatia Weledi wakati wa kufanya Upekuzi na Tathmini ya Mikataba mbalimbali ambayo Serikali inakusudia kuingia.

*"Katika kuhakikisha maslahi ya nchi yetu yanaendelea kuzingatiwa kwenye Mikataba itakayoingiwa ni lazima Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali-wawe na uwezo na ubobevu kwenye masharti ya Kimikataba yanayogusa sekta za kiuchumi na uwezo wa kusimamia mikataba hiyo".* Alisema Mhe. Rais.

Kwa upande wake Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kufanya Upekuzi na Tathmini kwenye Mikataba mbalimbali ambapo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Desemba 2024, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa imepekua Mikataba 1,799 na Hati za Makubaliano 352.

*"Kati ya mwezi Julai hadi Desemba 2024, jumla ya Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa 1,799 na Hati za Makubaliano (Memorandum of Understanding) 352 zilifanyiwa upekuzi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali."* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hatua nyingine, Mhe. Johari alisema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuwahimiza Mawakili wa Serikali na Wanasheria wote walioko katika utumishi wa umma kujiendeleza na kushiriki mafunzo ya fani mbalimbali ili waweze kufanya Upekuzi wa Mikataba na Hati za Makubaliano kwa ufanisi na ufasaha.

Aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Juma, awali akizungumza kabla ya kumkaribisha Mgeni rasmi, alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake anaoutoa katika kuimarisha Miundombinu ya Mahakama nchini.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari (wa kwanza kushoto) akipitia nyaraka mbalimbali wakati wa Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Sheria nchini, yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali, Jijini Dodoma.


Aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim H. Juma akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Sheria nchini, yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali, Jijini Dodoma.


Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno (kulia) na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice E. Mtulo (kushoto) wakifuatilia mijadala mbalimbali wakati wa Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Sheria nchini, yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali, Jijini Dodoma.

*"Nichukue nafasi hii kukushukuru Mhe. Rais na Serikali unayoiongoza kwa namna ambavyo umewezesha kuboreshwa kwa miundombinu mbalimbali ndani ya Mahakama, tunakushukuru sana kwa uwezeshaji wako mpaka sasa Mahakama tunaweza kutanua wigo wa kutoa haki kwa wananchi".*
Alisema Prof. Ibrahim H. Juma.

Vilevile, aliwakumbusha Watendaji mbalimbali wa Mahakama kufanya maboresho katika utendaji wao na kubadilika kifikra ili waweze kutoa huduma zenye ubora kwa wananchi.

*"Kila baada ya miaka mitatu tuna kawaida ya kufanya utafiti kutumia Taasisi ya nje ili kuona kama wananchi wanaridhika na huduma zetu, na kutuwezesha kuboresha zaidi huduma tunazozitoa."* Alisema Prof. Ibrahim Juma



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya Pamoja na baadhi ya Viongozi Waandamizi wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini, yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali, Jijini Dodoma.

# OWMS Kuendeleza Uhusiano na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

*Na Prisca Ulomi*



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (kushoto) akikabidhi Jarida la Wakili Mkuu kwa Rais wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mhe. Jaji Nestory Kayobera baada ya kikao baina yao kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Mahakama hiyo Jijini Arusha.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amekutana na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Rais wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki alipowatembelea kwa nyakati tofauti kwenye Ofisi zao zilizopo kwenye Mahakama hizo jijini Arusha.

Akizungumza na aliyekuwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Imani Daudi Aboud, Dkt. Possi alisema kuwa lengo la ziara yake ya kukutana na viongozi hao ni kuendeleza ushirikiano uliopo baina ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) na Mahakama hizo katika uendeshaji wa mashauri yanayoihusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwapa mafunzo ya kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali ya namna ya kujiandaa vizuri katika kuendesha mashauri ya kulinda maslahi mapana ya Tanzania. Pia, Mawakili waweze kupata uzoefu na uelewa wa namna ya kutunza, kusimamia na kuendesha mashauri kwa njia ya kidijitali na kuendeleza ushirikiano na azma ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga diplomasia.

Mhe. Rais Jaji Aboud alisema kuwa Mahakama yake iko tayari kuwapa nafasi Mawakili wa Serikali ya Tanzania kutoka OWMS kujifunza na kutumia Mahakama hii ili kujenga uwezo wao.

*"Tunatoa rai kwa Mawakili wa Serikali kutumia Mahakama hii kujenga uwezo na kufahamu uendeshaji wa Mahakama hii ili nchi iweze kunufaika kwa kuzingatia kuwa Mahakama hii ipo Arusha nchini Tanzania,"* alisisitiza Mhe. Rais Jaji Aboud.

Pia, Mhe. Rais Jaji Aboud aliongeza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wana nafasi kubwa ya kushauri Serikali kuhusu masuala ya kiufundi yanayohusu Sekta ya Sheria nchini na uendeshaji wa mashauri ya Serikali.

Katika hatua nyingine, Rais wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mhe. Jaji, Nestor K. Kayobera alisema kuwa Mahakama ya EAC imekuwa ikipokea Mawakili kutoka nchi wanachama ambao wamekuja kujifunza namna ya uendeshaji wa mashauri ya Mahakama hiyo. Hivyo, Mahakama ya EAC inatoa nafasi kwa Mawakili wa OWMS kuja kujifunza na hivi karibuni Mahakama Imenunua vifaa vya kisasa vya kidijitali vya masijala ya sheria na menejimenti ya mashauri.

*"Andaeni timu ya Mawakili wa Serikali na kuanzisha Kitengo maalum kinachoshughulikia mashauri ya nchi wanachama na Mawakili husika wajiandae ipasavyo katika uendeshaji wa mashauri husika,"* alisema Mhe. Jaji Kayobera, Rais wa Mahakama ya EAC.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alisema kuwa, *"ni muhimu kwa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuzingatia na kuangalia uwekezaji mbali mbali unaofanyika kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuhakikisha kuwa nchi hizi zinafikia maendeleo tarajiwa na kuwa makini katika uendeshaji wa mashauri yanayohusu uwekezaji. Mathalani miradi ya maendeleo ya Tanzania ya reli ya kisasa ya SGR na Bwawa la Uzalishaji Umeme la Mwalimu Nyerere ili miradi hiyo ifikie malengo tarajiwa na Ofisi iko tayari kutumia Mahakama kuwajengea uwezo Mawakili na kuendeleza ushirikiano uliopo".*

Akitoa salamu za shukrani kwa niaba ya Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mhe. Yohane Masara, Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki alisema kuwa anaishukuru OWMS kwa kuleta Mawakili wazuri wa Serikali katika uendeshaji wa mashauri ya EAC. Pia, alitoa rai kwa OWMS iendelee kuwajengea uwezo Mawakili wengine wengi zaidi ili wawe na uzoefu wa kutosha wa kuendesha mashauri.

Iliarifiwa kuwa, tangu kuanzishwa kwake, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu imesajili jumla ya mashauri 670, imemaliza mashauri 390 na inaendelea na uendeshaji wa mashauri 280. Tanzania ina mashauri 54 yanayoendeshwa kwenye Mahakama hiyo.



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akimkabidhi Jarida la Wakili Mkuu aliyekuwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Imani Aboud alipotembelea Mahakama hiyo kwa lengo la Kujitambulisha na kuona namna Mahakama hiyo inavyotekeleza majukumu yake Jijini Arusha.



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt Ally Possi (wa nne kushoto) na ujumbe wake akiwa kwenye picha ya pamoja na aliyekuwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Imani Aboud (wa nne kulia) baada ya kutembelea Mahakama hiyo kwa lengo la kujitambulisha na kujionea namna Mahakama hiyo inavyotekeleza majukumu yake jijini Arusha.

# "Tumieni Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao Ipasavyo."

*- Mhe. Naibu Waziri Mhandisi Maryprisca Mahundi*

*Na Rebecca Kwandu*

Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi ametoa rai kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka kote nchini, kutumia ipasavyo Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao wa mwaka 2025 uliozinduliwa hivi karibuni ambapo alisisitiza kuwa makosa ya kimtandao yamekuwa yakiongezeka katika jamii kutokana na kuongezeka kwa maendeleo ya teknolojia ambayo yameleta athari katika ukuaji wa uchumi na kuhatarisha utawala bora na haki za binadamu.

Naibu Waziri Maryprisca Mahundi aliyasema hayo wakati akizindua Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao wa mwaka 2025, katika hafla fupi iliyofanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Jijini Dodoma mnamo Februari 2025, pia amezitaja hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari za makosa ya kimtandao ikiwa ni pamoja na uandaaji wa miongozo mbalimbali juu ya matumizi bora ya mitandao, uundwaji wa vitengo mbalimbali katika taasisi za Serikali mahususi kwa ajili ya kushughulikia makosa ya kimtandao.

Aidha, uanzishaji na urekebishaji wa Sheria mbalimbali ili kudhibiti na kutoa adhabu dhidi ya matumizi mabaya ya mitandao zikiwepo Sheria ya Makosa ya Mtandao (The Cyber Crimes Act, 2015), Sheria ya Miamala ya Kielektoniki (Electronic Transaction Act, 2015) pamoja na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektoniki na Posta (Electronic and Postal Communication Act, 2010) sambamba na uundwaji wa kanuni mbalimbali.



Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi akikata utepe kuashiria Uzinduzi wa Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao uliofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma.

Aidha, alisema Serikali imekuwa ikishirikiana kwa ukaribu na vyombo vya kutoa huduma vinavyotumia mtandao, ndani na nje ya nchi ili kupambana na makosa ya mitandao nchini, hivyo mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao utawezesha Wapelelezi na Waendesha Mashtaka wanaoshughulikia kesi za kimtandao kote nchini kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kiwango kinachofanana.

*"Matumizi sahihi ya Mwongozo huo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti tatizo la ushughulikiaji usio sawa wa mashauri ya Mtandao, hususani katika vipengele vya Upelelezi, Uandaaji wa Hati za Mashtaka, Uendeshaji wa mashauri Mahakamani pamoja na uandaaji wa Hati nyingine zinazowasilishwa Mahakamani kwa kuwa makosa hayo huhusisha mbinu za kisasa ambazo zinahitaji umakini mkubwa katika kupeleleza na kuendesha kesi mahakamani"*. Alisisitiza Naibu Waziri.

Mhe. Mahundi ameipongeza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kufanikisha maandalizi ya Mwongozo na kusema ni matumaini yake kuwa utaleta mabadiliko makubwa katika utendaji wa kazi na hatimaye kuisaidia Serikali kufikia malengo yake ya kitaifa katika kudhibiti vitendo vya Makosa ya Kimtandao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu aliwashukuru wadau wanaofanya kazi na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ikiwemo Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Katiba na Sheria, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika maandalizi na uzinduzi wa Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao.

Alisema, Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Mtandao unalenga kuboresha utendaji kazi kwa kuweka namna iliyo sawa ya kushughulikia kesi za mtandao hivyo kuwawezesha Wapelelezi na Waendesha Mashtaka ya Makosa ya Kimtandao kushughulikia kesi za makosa ya kimtandao kwa ufanisi na tija.

Naye, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo alisema, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imesimama kama kiongozi katika kuandaa Mwongozo huo, ikiwa ni pamoja na kutambua ushirikiano mkubwa walioupata kutoka kwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi na Wizara anayoiongoza.

*"Hili linatupa faraja ya kuona kwamba shughuli ya kupambana na uhalifu wa kimtandao haipo kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka peke yake na hivyo inatupa dhamira ya dhati ya kupambana na uhalifu wa kimtandao na kwa pamoja tunaunganisha nguvu zetu ili kupambana na uhalifu huo."* Alisema Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka.

Uandaaji wa Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Mtandao umezingatia maeneo yenye changamoto za utendaji wa kila siku katika eneo la makosa ya mtandao kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka Ili kuondokana na dosari za kiutendaji wakati wa kushghulikia makosa ya jinai katika maeneo ya upelelezi na uendeshaji wa Makosa ya Kimtandao. Mwongozo huo ulizinduliwa tarehe 13 Februari, 2025 katika ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi akikabidhi Miongozo kwa Mkurugenzi wa Sheria wa TAKUKURU Bw. George Barasa mara baada ya kushiriki kwenye Hafla ya Uzinduzi wa Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao Iliyofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Hafla ya Uzinduzi wa Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Makosa ya Kimtandao iliyofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma.



# Uzinduzi na Utiaji Saini wa Sheria Zilizofanyiwa Urekebu Toleo la Mwaka 2023

*Na Leila Muhaji*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kukamilisha zoezi la Urekebu wa Sheria na kuifanya Serikali ya Awamu ya Sita kuingia katika historia ya kuandika Juzuu mpya za Urekebu.

Mhe. Rais Dkt. Samia alitoa pongezi hizo wakati akihutubia viongozi na wageni mbalimbali waliohudhuria hafla ya utiaji saini tamko la Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la Mwaka 2023 iliyofanyika Ikulu Chamwino, Jijini Dodoma tarehe 23 Aprili, 2025.

*"Tunatoa Shukrani zetu kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kulikamilisha hili na kuifanya Serikali ya Awamu ya Sita kuingia kwenye historia ya kuandika Juzuu mpya za Urekebu."* Alisema Rais Samia**.**

Aidha, Mhe. Rais alisema kuwa kukamilika kwa zoezi la Urekebu wa Sheria ni hatua muhimu katika maendeleo ya Taifa, kwakuwa upatikanaji wa Sheria zilizowekwa wazi na zinazoendana na wakati kutasaidia kuwepo kwa amani na shughuli za kiuchumi kufanyika kwa urahisi.

*"Sheria ni kioo cha ustaarabu wa taifa, kukamilika kwa toleo hili ni hatua muhimu katika ustawi wa maendeleo ya taifa letu."* Alisema Mhe. Rais

Mhe. Rais alisema kuwa, kukamilika kwa Juzuu hizo za Sheria kutasaidia kufanya utafiti na kupata uhakika wa Sheria inavyosema, hivyo kurahisisha maamuzi na kupelekea upatikanaji wa haki kwa wananchi na kwa wakati.

*"Juzuu hizi zilizorekebishwa ni muhimu sana katika kuongeza uwazi na zitazidi kuongeza imani ya wananchi kwa Serikali yao."* Alisema Mhe. Rais

Katika hatua nyingine, Rais Samia aliiagiza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha kuwa inazitafsiri Juzuu za Sheria kwa lugha ya Kiswahili ili wananchi waweze kuzisoma na kuzielewa, ili kusaidia wananchi kutambua haki zao na kusaidia kupunguza migogoro mbalimbali.

Kwa upande wake, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) alitoa pongezi kwa Mhe. Rais na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kufadhili mradi huo mkubwa wa Urekebu wa Sheria mbalimbali nchini, ambapo mradi huo umetumia Rasilimali fedha na watalaamu wa ndani ya nchi.

*"Mhe. Rais nakupongeza kwakuwa mradi huu mkubwa wa Urekebu wa Sheria uliofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali umetekelezwa kwa kutumia fedha za ndani."* Alisema Mhe. Majaliwa

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari akizungumza katika hafla hiyo alisema kuwa, zoezi la Urekebu wa Sheria, ni urithi wa Kisheria kwa wadau wa Sekta ya Sheria, wadau wa haki na wadau wa utawala bora kwakuwa Sheria ni msingi wa haki, amani na maendeleo.

Vilevile, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Awamu ya Sita kwa ujumla kwa kufadhili zoezi hilo kwa kutoa fedha na kuijengea uwezo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na kwa kuwajengea uwezo wataalamu waliofanikisha zoezi hilo.

*"Kwa namna ya pekee naomba kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Serikali yako kwa kuwezesha mradi huu wa Urekebu. Hii ni mara ya kwanza kwa mradi huu kufanyika kwa fedha za ndani na Wataalamu wa ndani."* Alisema Mhe. Johari

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa, kutokana na mageuzi na jitihada mbalimbali zilizofanyika katika usimamizi wa Sheria na maboresho ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yamechagiza kwa kiasi kikubwa kukamilika kwa zoezi la Urekebu wa Sheria.

*"Maboresho ya kuajiri zaidi ya Mawakili wa Serikali 50 na kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria ni hatua muhimu iliyopelekea kukamilika kwa zoezi hili."* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Tamko la Sheria zilizofanyiwa Urekebu lililosainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan zilianza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2025.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akizungumza wakati wa halfa ya Utiaji saini Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la mwaka 2023. Hafla hiyo ya Utiaji saini ilifanyika Ikulu Chamwino, Jijini Dodoma.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akizungumza wakati wa halfa ya Utiaji saini Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la mwaka 2023. Hafla hiyo ya Utiaji saini ilifanyika Ikulu Chamwino, Jijini Dodoma.

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yafanikiwa Kuokoa Zaidi ya Shilingi Trilioni 3.6

*— Na Prisca Ulomi*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) ilianzishwa kupitia Hati Idhini (Instrument) ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotolewa kwa mujibu wa Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kutangazwa tarehe 13 Februari, 2018 katika Gazeti la Serikali Na. 50 la Mwaka 2018.

Uanzishwaji huo ulitokana na marekebisho ya Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Office of the Attorney General (Re-structure) Order, 2018 under GN. No. 48 of 2018) ambapo ilipelekea kuanzishwa kwa Ofisi tatu ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Lengo la kuanzishwa kwa Ofisi hii lilikuwa ni kuimarisha uwezo wa Serikali katika kuratibu, kusimamia, kushauri na kuendesha mashauri yote ya madai ikiwemo mashauri ya haki za binadamu, katiba, uchaguzi na mashauri ya usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali au dhidi yake ndani na nje ya nchi. Pia, kuendesha mashauri ya taasisi binafsi pale ambapo mashauri hayo yana maslahi ya umma au yanayohusu mali ya umma. Hii inajumuisha kuiwakilisha Serikali katika Mahakama zote za ndani na nje ya nchi na katika Mabaraza ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kitaifa na Kimataifa.

Katika kutekeleza jukumu hili, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeshughulikia mashauri ya madai 12,878 yaliyohusisha Serikali na taasisi zake na kumaliza mashauri 5,065. Baada ya kumaliza mashauri hayo, Serikali imeokoa kiasi cha shilingi trilioni tatu bilioni sitini na moja milioni mia moja kumi na sita, laki nne tisini na saba, mia tisa thelathini na nane na senti thelathini na mbili (3,061,116,497,938.32) na dola za Marekani milioni hamsini na tano (USD 55,000,000).

Aidha, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeshughulikia mashauri ya usuluhishi mia tatu kumi na tano (315) yaliyohusisha Serikali na



Mawakili wa Serikali kutoka mikoa mbalimbali nchini wakiwa katika Mkutano Mkuu ulioandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano AICC, jijini Arusha.

kwa kumaliza mashauri hayo, Serikali imeokoa kiasi cha shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia mbili na tano, laki 8, mia nne na kumi (12,205,800,410) na dola za Marekani bilioni moja, milioni mia tano arobaini na nane, laki tano thelathini na nne na mia nane arobaini na saba. (USD 1,548,534,847).

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Novemba, 2020 hadi Machi, 2025; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuanzisha Ofisi za mikoa kumi (10) zaidi ikilinganishwa na Ofisi nane (08) za mikoa ambazo zilianzishwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2018/2019 katika mikoa ambayo ina masijala zenye Mahakama Kuu. Lengo la kuanzishwa kwa Ofisi hizo ni kusogeza huduma za uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi karibu na Mahakama Kuu ili kufanikisha kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa ufanisi.



Daraja la Kigongo-Busisi ni mojawapo ya madaraja ya kihistoria nchini Tanzania, likiwa ni mradi mkubwa wa miundombinu unaotarajiwa kubadilisha maisha ya wananchi kwa kiwango kikubwa na kuinua uchumi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa Tanzania.



Barabara ya Nyamuswa–Bulamba ni ushahidi wa maendeleo na uunganishaji wa jamii katika Mkoa wa Mara. Barabara hii ambayo hapo awali ilikuwa ya vumbi na isiyopitika, sasa imebadilika na kuwa njia muhimu inayounganisha miji, masoko, shule, na vituo vya afya.




Ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR unawawezesha wananchi kupata huduma ya usafiri ya haraka, uhakika na ya kisasa hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na kuchochea maendeleo katika nyanja ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa taifa la Tanzania.

Uokoaji wa fedha hizo umeiwezesha Serikali kujikita katika kuanzisha miradi ya maendeleo katika Sekta ya Ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara na madaraja.

# Ziara ya Viongozi, Wa Haki Jinai Katika Magereza Yaleta Mafanikio Mkubwa

*Na Rebecca Kwandu*

Viongozi, Wadau wa Haki Jinai kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa pamoja wamefanya ziara katika Magereza ya Keko, Segerea na Ukonga kusikiliza kero na changamoto za Mahabusu waliopo katika Magereza hayo kwa lengo la kuwasikiliza na kushughulikia changamoto na kero zinazowakabili Mahabusu na Wafungwa ikiwepo kero ya uchelewashaji wa Upelelezi.

Katika ziara hiyo iliyofanyika kuanzia tarehe 18 hadi 20 Novemba, 2024 Mkurugenzi wa Mashtaka aliongozana na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Bw. Crispin Chalamila, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Bw. Aretas Lyimo na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai nchini Bw. Ramadhan Kingai.

Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu alieleza kuwa ziara hiyo ya viongozi na mazungumzo yaliyofanyika kati ya viongozi hao na Mahabusu katika Magereza hayo yamekuwa yenye manufaa makubwa. kwa kuwa sio tu imesaidia kurekebisha na kuboresha utendaji wa kazi, bali pia imesaidia kupunguza msongamano wa Wazuwiwa Gerezani.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo wa Magereza, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Bw. Aretas Lyimo alitoa onyo kwa watuhumiwa wanaoachiwa au kumaliza vifungo vyao kutorudia kutenda makosa bali wasaidiane na Serikali katika kuiletea nchi maendeleo na kufanya kazi halali ili kujiongezea kipato.




Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Bw. Crispin Chalamila, Kamishna Generali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Bw. Aretas Lyimo wakiwa na viongozi wa ngazi ya mkoa wanaounda mnyororo wa Haki Jina, Waendesha Mashataka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka mara baada ya kutembelea Gereza Kuu Ukonga Jijini Dar es salaam.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Bw. Crispin Chalamila alisema lengo kuu la ziara waliyoifanya ilikuwa ni kupokea changamoto zinazowakabili watuhumiwa waliopo katika Mahabusu kwa lengo la kuchukua hatua za kushughulikia changamoto zilizowasilishwa ili haki itendeke na ionekane ikitendeka.

Naye, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Bw. Ramadhani Kingai alisema kuwa, baada ya kuzungumza na wafungwa na mahabusu katika ziara hiyo atahakikisha wanaweka mikakati madhubuti ya kutatua changamoto za kiupelelezi ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati.

Naye, Mkuu wa gereza la Mahabusu la Keko, Kamishna Msaidizi Juma Mgumba alimshukuru Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu na timu aliyoambatana nayo katika ziara hiyo, alisema upelelezi ukikamilishwa mapema na kesi zikisikilizwa na kuisha kwa wakati itasadia watuhumiwa kujua hatma yao na msongamano katika gereza hilo kupungua au kuisha kabisa.




Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Bw.Ramadhani Kingai Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Bw. Crispin Chalamila, Kamishna Jenerali wa Mamlak ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Bw. Aretas Lyimo wakiwa na viongozi wa ngazi ya mkoa wanaounda mnyororo wa Haki Jinai, Waendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka mara baada ya kutembelea gereza la Mahabusu Keko Jijini Dar es salaam.



Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Bw. Ramadhani Kingai, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Bw. Crispin Chalamila, Kamishna Jenerali wa Kupambana na Dawa za kulevya Bw. Aretas Lyimo na viongozi wa ngazi ya mkoa wanaounda mnyororo wa Haki Jinai, Waendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakifuatilia taarifa ya hali ya Magereza kutoka kwa Mkuu wa Gereza la Keko Jijini Dar es salaam.

# “Tunataka kuwa Champion wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050” - Mwanasheria Mkuu wa Serikali

*Na Leila Muhaji*

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari amesema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshiriki kikamilifu katika kutoa maoni ya utengenezaji na uandaaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ili kuhakikisha kuwa Dira hiyo inaakisi masuala yote ya Sekta ya Sheria.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyasema hayo, katika mahojiano maalum na Vyombo vya Habari yaliyofanyika Ofisini kwake, Mtumba Jijini Dodoma.

Aidha, Mhe. Johari alieleza kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba mambo yote yanayoihusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanatekelezwa ipasavyo ili kuweza kufikia malengo ya Dira 2050.

*"Sisi kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutahakikisha kwamba tunaoanisha vizuri Sheria zetu tulizonazo na kule tunakotaka kwenda, ni lazima tuwe na legal framework ya kutufikisha."* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Pia alisisitiza suala la kufanya maboresho katika Sheria mbalimbali ili ziweze kuendana na mabadiliko ya Kijamii na Kiuchumi pamoja na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji wa Sheria.

*"Sisi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunataka kuwa Champion kwa kuhakikisha kuwa sheria zetu zote tunazioanisha na Dira 2050."* Alisema

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliongelea suala la Ufasiri wa Sheria, ambapo alisema, Sheria mbalimbali zimeweza kutafsiriwa kutoka lugha ya Kingereza kwenda Kiswahili ili ziweze kutumika kwa urahisi na watumiaji.

*"Kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2024 tumeweza kutafsiri jumla ya Sheria kuu 300 lengo kubwa ikiwa ni kuwarahisishia watumiaji wa Sheria."* Alieleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Sambamba na hilo, Mhe. Johari alisema kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeweza kukamilisha



zoezi la Urekebu wa Sheria, ambapo Sheria mbalimbali zilizorekebishwa zimeweza kufanyiwa Urekebu, hivyo watumiaji wa Sheria watapata Sheria hizi zikiwa zimerekebishwa kwa wepesi zaidi.

Aidha, Mhe. Johari alisema kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kutoa huduma za Ushauri wa Kisheria bila malipo kwa wananchi kwa kushirikiana na Kamati za Ushauri wa Kisheria zilizoko katika ngazi ya Mikoa na Wilaya.

Alieleza kuwa, kufanyika kwa Kliniki hizo ni mojawapo ya hatua za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika azma ya kusogeza huduma za Kisheria karibu zaidi na Wananchi.

*"Lengo kubwa la Kliniki hizi ni kusogeza huduma za kisheria karibu na Wananchi, huku tukitimiza matakwa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akisisitiza umuhimu wa kusogeza huduma kwa wananchi."* Alisema Mhe. Johari.

Pia, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa kupitia Kliniki za Kisheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeweza kutatua changamoto za Kisheria zinazowakabili wananchi katika mikoa mbalimbali, huku akiyataja masuala ya Ardhi, Mirathi, Ajira, Unyanyasaji wa Kijinsia kuwa ni masuala yanayojitokeza mara kwa mara wakati wa kuhudumia wananchi kupitia Kliniki hizo.

*"Tumeweza kufanya Kliniki hizi katika Mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro na Mwanza ambapo jumla ya Wananchi 1,845 wameweza kupata huduma za Ushauri wa Kisheria bure kutoka kwa timu ya wataalamu wetu."* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na viongozi waandamizi wa Serikali wakati wa hafla ya Uzinduzi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 iliyofanyika Jijini Dodoma.

# Wakili Mkuu wa Serikali Awafunda Mawakili wa Serikali Uendeshaji wa Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

*—— Na Prisca Ulomi ——*



Wakili Mkuu wa Senkali, Dkt. Ally A. Possi akifungua mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu Sheria na Taratibu za Uendeshaji wa Mashauri ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yaliyofanyika mkoani Morogoro.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amefungua mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kwa lengo la kuwajengea uwezo Mawakili hao kuhusu namna bora ya kuendesha mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa yanayotarajiwa kufunguliwa baada ya kuhitimishwa kwa uchaguzi uliofanyika nchi nzima tarehe 27 Novemba, 2024.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo, Dkt. Possi alisema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa kwa niaba ya Serikali na taasisi zake kwenye Mabaraza na Mahakama ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku mbili na yalitolewa na wakufunzi wabobezi wa Sekta ya Sheria ili kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali kwenye maeneo mbalimbali yanayohusu kanuni na taratibu za uendeshaji wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

*"Tumeona ni muhimu kuendesha mafunzo haya ili kuwakumbusha Mawakili wa Serikali kanuni na taratibu zote za uendeshaji wa mashauri yanayohusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa yatakayofunguliwa ili waweze kuyasimamia kwa weledi na kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati,"* Alisema Dkt. Possi.

Alieleza kuwa ili kulinda haki za msingi za watanzania wote kwa mujibu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na kupitia kanuni ya 44 ya Kanuni za Uchaguzi wa Wenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za mwaka 2024, kanuni ya 41 ya Kanuni za Uchaguzi wa Wenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo za mwaka 2024, kanuni ya 44 ya Kanuni za Uchaguzi wa Wenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za mwaka 2024, na kanuni ya 43 ya Kanuni za Uchaguzi wa Wenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za mwaka 2024 zimeweka wazi kuwa mgombea yoyote ambae hakuridhika na matokeo ya uchaguzi au uendeshaji wa uchaguzi kuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya siku thelathini tangu siku ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi husika.

Dkt. Possi aliongeza kuwa iwapo mgombea yeyote atafungua shauri la uchaguzi, shauri hilo litafunguliwa dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri husika au afisa aliyeteuliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataunganishwa kwenye shauri hilo.

Dkt. Possi alieleza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itakuwa na jukumu la kusimamia na kuendesha mashauri ya uchaguzi kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wowote ambapo mlalamikaji atafungua shauri la uchaguzi Mahakamani.

Mafunzo hayo yalijikita kwenye mada mbalimbali ikiwemo uelewa wa jumla wa sheria zinazosimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania (General Overview of the Laws Governing Local Government Election In Tanzania), Taratibu za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Understanding Election Procedures for Local Government Authorities), maadili kwenye uendeshaji. wa mashauri ya uchaguzi (Ethical Issues In Handling Election Petitions), taratibu za uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi (Election Petitions Handling Mechanism: Filing of Pleadings and Hearing), Utafiti kwenye uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi (The Role of Research in Handling Election Petitions for Local Government Election); na ushahidi wa kieletroniki kwenye uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi (Electronic Evidence in Election Petitions: Law And Practice).

> ***"Hivi Karibuni, nilitembelea Mahakama Kuu Geita, kujionea Mahakama mtandao, wenzetu wapo katika hatua ya kuachana na matumizi ya karatasi na kila kitu kinaendeshwa kwa TEHAMA.***

Dkt. Possi alisema kuwa Serikali iliona ni muhimu kuwajengea uwezo Mawakili hao kwa kutoa mafunzo hayo baada ya kupata maoni ya wadau wa Sekta ya Sheria nchini ikiwemo Mahakama ya Tanzania kuhusu maeneo yanayopaswa kuboreshwa katika kutekeleza majukumu ya OWMS ya kuiwakilisha Serikali Mahakamani na kwenye Mabaraza mbalimbali katika uendeshaji wa mashauri ikiwemo mashauri yanayohusu uchaguzi hususani uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka 2024.



Baadhi ya Mawakili wa Serikali wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu Sheria na Taratibu za Uendeshaji Mashauri Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yaliyofanyika mkoani Morogoro.

Aidha, Dkt. Ally Possi alitoa rai kwa Mawakili hao kuwa wasikivu wakati wa mafunzo hayo kwa kuwa ni matarajio yake kuwa baada ya mafunzo hayo Mawakili hao watapata uelewa wa kina kuhusu Kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kanuni za uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na uendeshaji wa mashauri kwa ujumla ili waweze kuendesha mashauri ya uchaguzi kwa ufanisi, weledi na ujuzi na kuboresha usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya Serikali kwa kuzingatia utafiti, misingi ya uandaaji wa nyaraka za Mahakama, uandaaji wa mashahidi, namna ya kutoa ushahidi wa kielektroniki na masuala mengine. yanayohusu uendeshaji wa mashauri kwenye Mahakama.

Katika hatua nyingine, Dkt. Possi aliwataka watumishi hao kufanyia kazi yote watakayoelezwa sambamba na kuzingatia Kanuni na Maadili ya Utumishi wa Umma wakati wote katika kusimamia na kuendesha mashauri ya uchaguzi huku wakiendelea kuzingatia matumizi ya TEHAMA katika kusimamia mashauri hayo.

*"Hivi Karibuni, nilitembelea Mahakama Kuu Geita, kujionea Mahakama mtandao, wenzetu wapo katika hatua ya kuachana na matumizi ya karatasi na kila kitu kinaendeshwa kwa TEHAMA, nafikiri ni wakati sasa na sisi tuanze kuelekea huko kwani dunia haitusubiri"*, alisema Dkt. Possi.



Baadhi ya Mawakili wa Serikali wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu Sheria na Taratibu za Uendeshaji Mashauri Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yaliyofanyika mkoani Morogoro.

Akitoa salamu za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo, Mkurugenzi wa Idara ya Madai, ndugu Mark Mulwambo alisema kuwa, mafunzo hayo ni mwendelezo wa mipango ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mawakili wa Serikali waliopewa hati idhini ya kuendesha mashauri ya Serikali kwa niaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Mawakili wa Serikali wa kutoka Wizara na taasisi mbali mbali za Serikali.

# Mkurugenzi wa Mashtaka Awataka Waendesha Mashtaka Kuwa Mfano wa Kusimamia Haki

*Na Rebecca Kwandu*




Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akifungua kikao kazi na Mafunzo ya Nadharia na vitendo kwa Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi kilichofanyika Mkoani Pwani.

Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi wametakiwa kuwa mfano katika kusimamia haki na kujenga imani kwa wananchi kwa kuhakikisha kuwa haki inatendeka wakati wa uendeshaji wa mashauri.

Mkurugenzi wa Mashtaka, Bw. Sylvester Mwakitalu aliyazungumza hayo wakati akifungua mafunzo ya nadharia na vitendo kwa Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi yaliyofanyika mkoani Pwani. Alisema Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ina dhamira ya dhati ya kuona kuwa inakuwa mfano katika kusimamia haki kwa kujenga imani kwa wananchi na jamii nzima kwa ujumla pamoja na kuhakikisha haki, amani na usalama vinatamalaki katika jamii.

*"Tujenge imani kwa jamii na kwa wananchi, jambo la mwananchi likiwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wajue kuwa halihitaji kutoa chochote bali waamini kwamba haki itatendeka, jambo hili litafanikiwa kama ninyi mnaoamua kushtaki ama kutokushtaki mtatenda kwa haki na kutokukubali kutumika iwe kwa maslahi binafsi ama ya watu wengine".* alisisitiza Mkurugenzi wa Mashtaka.

Alisema Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imepewa jukumu kubwa na nyeti linalogusa haki za watu kwa kuwa watendaji wake wanahusika na kutoa maamuzi ya kushtaki na wakati mwingine maamuzi ya kutokushtaki na hayo yote yanagusa haki za watu na kwasababu hiyo wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa weledi wa hali ya juu na kwa uaminifu.

Aidha, Mkurugenzi wa Mashtaka alieleza kuwa, timu ya menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeweka mikakati mingi ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa watumishi kupitia mafunzo ya muda mfupi, mafunzo ya vitendo na mafunzo ya muda mrefu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ukamilifu na kuweza kuwahudumia wananchi ambao wanaangukia kwenye eneo lao husika la kimashtaka.

Alieleza kwamba mojawapo ya mikakati inayotekelezwa na Ofisi ni pamoja na kuwapa mafunzo Wakuu wa Mashtaka Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi kwa kuwa wao ndiyo nguzo muhimu kwenye utekelezaji wa majukumu ya mashtaka.

*"Waendesha Mashtaka Viongozi na Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya ndio nguzo yetu, tunawategemea kwa kiasi kikubwa sana katika kuwahudumia wananchi kwenye eneo la kimashtaka. Sisi kama ofisi matumaini na matarajio yetu makubwa kabisa yapo kwenu, hivyo nawataka mfahamu na mlitambue hilo."* Alibainisha Mkurugenzi Mwakitalu.

Aidha, aliwataka washiriki kuongeza ushirikiano na wadau wa Haki Jinai ili kupata matokeo chanya katika uendeshaji wa mashauri ya jinai.

Kwa upande wake, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo alisema mafunzo hayo ni ya kipekee na ya muhimu kwani yamebeba nadharia na vitendo na pia yamelenga kusaidia kuwaongezea ujuzi katika utendaji wao kazi na kuwasaidia kufanya maamuzi sahihi ya kushtaki.

*"Tupo hapa kwa lengo la kupata mafunzo yaliyobeba nadharia na vitendo ili kukumbushana baadhi ya mambo ya muhimu sana kwenye uratibu na usimamizi wa upelelezi pamoja na uendeshaji wa mashtaka ambalo ndio jukumu kubwa tulilokasimiwa na Katiba ya nchi pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan."* Alibainisha Naibu DPP.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Simon Ntobbi aliwataka washiriki hao kwenda kutoa elimu kwa watumishi ambao hawakupata fursa ya kushiriki mafunzo hayo.

*"Tunataka mashauri yaweze kushughulikiwa kwa wakati na ushindi wa kesi uongezeke kwa kufuata misingi ya haki."* Alisema Mkurugenzi Ntobbi.





Washiriki wa Kikao kazi na Mafunzo ya Nadharia na Vitendo kwa Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi wakifuatilia kwa umakini mada mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kikao hicho kilichofanyika Mkoani Pwani.

# Mabadiliko ya Sekta ya Sheria: Nguzo Muhimu ya Dira ya Maendeleo 2050

*Na Leila Muhaji*

Wakati nchi ikijiandaa kuanza utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050 kuanzia Julai mwakani, sekta ya sheria inaendelea kupitia mageuzi makubwa, yakijijenga si tu kama msingi wa utawala bora pia kujenga jamii na uchumi imara, bali pia moja ya nyenzo za utekelezaji wa Dira hiyo.

Kutoka kwenye matumizi ya teknolojia na upatikanaji wa haki hadi ukuaji wa taasisi, ufanisi wa kifedha na uongozi wa kikanda, taarifa za hivi karibuni zinaonyesha mfumo wa sheria unaoacha uendeshaji wa kizamani na kuwa mfumo wa kisasa unaotumia teknolojia kama injini ya kutoa huduma kwa umma. Mageuzi ya kihistoria Katika kile ambacho wataalamu wa sheria wanakiita mafanikio ya kihistoria, serikali ilikamilisha uchapishaji wa Toleo la Marejeo la Sheria za Tanzania la mwaka 2023, ambalo linajumuisha na kutafsiri sheria kuu 446 kwa lugha ya Kiswahili - lugha rasmi ya taifa.

Jambo hili si geni kwani imeshazoeleka nchini kuwa Sheria zinaandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Toleo hili jipya la sheria za nchi, ambalo lilianza kutumika rasmi Julai 1, 2025, ndilo la kwanza kuandikwa kwa gharama za serikali bila msaada kutoka Benki ya Dunia au wafadhili wa nje kama ilivyozoeleka. Umuhimu wa jambo hili ni kuwa toleo hilo jipya la sheria linatoa nafasi ya demokrasia ya kisheria kwa wananchi wengi, ambao sasa wanaweza kuelewa sheria kupitia lugha wanayoifahamu vema.

*"Umiliki wa sheria huanza na lugha. Hii itasaidia kupunguza pengo kati ya sheria na wananchi,"* alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Hamza Johari, aliyesimamia mchakato huo Kuanzia 2021 hadi 2025, Tanzania pia imetunga au kurekebisha sheria kuu 57 na zaidi ya nyaraka 4,000 za kisheria, jambo lililoboresha mfumo wa sheria katika maeneo kama fedha, mazingira, ardhi na uchumi wa kidijiti.

Teknolojia na upatikanaji wa haki Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, iliyoanzishwa chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, ni mojawapo ya nguzo za mabadiliko haya. Chini ya kampeni hii vituo vya msaada wa kisheria vilianzishwa katika mikoa 25. Vituo hivi vimewasaidia moja kwa moja watu milioni 2.7, huku zaidi ya watanzania milioni 6.4 wakipata elimu ya sheria kupitia mikutano na majukwaa ya umma.

Wakati huo huo, ushirikiano wa Tanzania na taasisi ya Laws Africa na GIZ uliwezesha kuzifanyia mabadiliko makubwa asilimia 40 ya sheria ambazo sasa zinaendana na teknolojia ya kidijiti. Kazi hii ilifanyika hadi mwisho wa 2023 kupitia jukwaa la Indigo. Maelfu ya sheria hizo, pamoja na hukumu za mahakama, sasa zinapatikana sasa bila malipo kupitia Tanzania Legal Information Institute (TanzLII). Ilipangwa kuwa hadi kufikia Juni 2025, TanzLII iwe imechapisha hukumu 65,815 ili kuvutia watumiaji milioni 2.6. Mabadiliko haya hayajaleta mafanikio ndani ya nchi pekee




Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari akimsikiliza mmoja wa Wananchi wakati wa Kliniki ya Sheria bila malipo Mkoani Singida.



Baadhi ya Wananchi wakipata huduma za Ushauri wa Kisheria wakati wa Kliniki ya Sheria bila Malipo kwa wananchi wa mkoa wa Singida.

Kwa upande mwingine yamezivutia nchi nyingine za Afrika maofisa kutoka Ghana na Nigeria walitembelea Tanzania mwezi Juni 2025 kujifunza mfumo huo.

Ujenzi wa miundombinu ya sheria Mageuzi ya sheria yanaambatana na uwekezaji wa moja kwa moja katika miundombinu na rasilimali watu. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa idadi ya majaji imeongezeka kutoka 92 mwaka 2021 hadi 146 mwaka 2025 huku idadi ya mahakimu nayo ikipanda kutoka 1,412 hadi 1,426. Aidha, ujenzi wa vituo sita vya Haki Jumuishi (IJCs) umekamilika katika miji kama Dodoma na Mwanza, huku vituo tisa zaidi vikiwa katika hatua mbali mbali za ujenzi. Sambamba na hatua hiyo, mahakama nyingi za wilaya na msingi zimejengwa au kuboreshwa, hasa vijijini.

Hatua hizi zimepunguza mrundikano wa kesi, kuboresha upatikanaji wa haki na kuiweka Tanzania katika nafasi ya uongozi wa maendeleo ya miundombinu ya haki katika ukanda huu. Mafanikio yaokoa fedha Nje ya mahakama, taasisi za kisheria pia zimeleta faida kubwa kifedha. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ilitatua kwa mafanikio kesi 966 zikiwamo 814 za ndani na moja ya kimataifa na kuokoa kiasi cha TSh bilioni 232.7 (zaidi ya dola milioni 100), ambazo zingetumika iwapo kesi hizo zingeendeshwa kwa mfumo wa kawaida.

Haya ni matokeo ya mikakati bora ya kupunguza hatari, ushauri wa mapema wa kisheria na taaluma bora ya mawakili wa serikali wanaopatiwa mafunzo chini ya mpango mpya wa "Legal Excellence for Tomorrow". Mpango huo pia unahusisha uanzishwaji wa mfumo mpya wa Usimamizi wa Kesi (CMIS), maktaba ya sheria mtandaoni na tovuti ya kisasa ya mawakili wa serikali.

Uongozi wa kikanda Mafanikio ya Tanzania katika sekta ya sheria yanazidi kutambuliwa na nchi nyingine barani Afrika. Mbali na kupokea wageni kutoka Afrika Magharibi, nchi pia inaongoza mijadala ya bara kuhusu upatikanaji wa sheria kwa uwazi, mifumo ya kidijitali ya mahakama na haki kwa wote

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi, wameunganisha juhudi za kisasa za sheria na Dira ya Maendeleo 2050, wakihimiza wataalamu wa sheria kuoanisha mifumo ya kisheria na malengo ya taifa kama vile uanzishaji wa viwanda, kuvutia uwekezaji na kukuza uchumi wa kidijitali.
*"Sekta ya Sheria lazima iwe kitovu cha maendeleo ya taifa - si pembeni,"* alisisitiza Mhe. Johari kwenye mkutano wa kikanda huko Arusha.

Kwa nini ni muhimu? Mabadiliko haya hayahusu mahakama pekee, bali yanahusisha ujenzi wa mfumo wa sheria unaolinda haki, kuvutia wawekezaji, kujenga imani ya wananchi na kuhimiza maendeleo jumuishi. Kwa wafanyabiashara, hii inamaanisha sheria zilizo wazi, utatuzi wa migogoro kwa haraka na mazingira yanayotabirika. Hali hii inachochea sana uwekezaji na biashara kutoka nje ya nchi. Kwa wananchi, inamaanisha kuwa sasa watakuwa wanapata haki karibu na mahali wanapoishi. Hawalazimiki tena kusafiri umbali mrefu kutafuta haki zao. Kwa bara la Afrika, Tanzania inazidi kuwa mfano wa mageuzi ya sheria yaliyojengwa kwa lugha ya wananchi, yanayoendeshwa na teknolojia, na yanayoleta matokeo kwa jamii.

Kadri Dira ya Maendeleo 2050 inavyopiga hatua, sekta ya sheria inaweza kuwa injini tulivu ya mafanikio hayo - ikiweka viwango vya uwazi, usawa na ufanisi katika utawala na usimamizi wa maendeleo ya kiuchumi.

# Wakili Mkuu wa Serikali Akutana na Mkurugenzi wa Benki ya Dunia

*Na Prisca Ulomi*

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amekutana na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia nchini Tanzania anayesimamia nchi za Malawi, Zambia na Zimbambwe, Ndugu Nathan Belete kwa lengo la kujadiliana namna ya kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili katika maeneo mbalimbali ya kisheria na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Katika mazungumzo yao, viongozi hao walijadili fursa za kushirikiana katika kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali na watumishi wengine kupitia mafunzo ili kuimarisha utendaji kazi katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali kwa ufanisi zaidi.

Aidha, Dkt. Possi aliiomba Benki ya Dunia kuangalia uwezekano wa kuiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa na miradi ya maendeleo mathalani inayohusu ujenzi wa majengo ya Ofisi katika kila mkoa ambapo kuna Mahakama Kuu ya Tanzania ili kupanua wigo wa uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi nchini.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amesisitiza kuwa upo umuhimu wa kupanua miundombinu ya Ofisi kwa kujenga majengo ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika mikoa mbalimbali nchini ili kuhakikisha kuwa huduma zinawafikia wananchi kwa urahisi.

Benki ya Dunia imeonesha utayari wa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuhakikisha kuwa Mawakili wa Serikali wanapata mafunzo bora yanayolingana na viwango vya kimataifa. Kwa upande wake Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia Tanzania anayesimamia nchi za Malawi, Zambia na Zimbabwe, ndugu Nathan Belete alipongeza juhudi zinazofanywa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na kuahidi kuendelea kushirikiana na Ofisi hiyo katika kutafuta njia bora za kufanikisha miradi ya maendeleo inayolenga kuimarisha mfumo wa sheria nchini.

Aliongeza kuwa Ofisi yake iko tayari kuhakikisha kuwa Mawakili wa Serikali wanapata mafunzo bora yanayolingana na viwango vya kimataifa ili kuhakikisha wanaendelea kusimamia mashauri kwa weledi hasa katika kada za mafuta na gesi ili kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika kusimamia rasilimali za nchi. Ziara ya Wakili Mkuu wa Serikali ni mfululizo wa ziara ambazo amekuwa akifanya kwa lengo la kuimarisha na kuongeza ushirikiano na taasisi nyingine ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali kuhakikisha kuwa Sekta ya Sheria na usimamizi wa mashauri inaendeshwa kwa ufanisi unaoendana na viwango vya kimataifa kwa manufaa ya taifa.




Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama kushoto) akisalimiana na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia anayesimamia nchi za Tanzania, Malawi, Zambia na Zimbabwe, ndugu Nathan Belete baada ya kuwasili Ofisini kwake Jijini Dar es Salaam.

# Jaji Mkuu Apongeza Taasisi Zinazounda Utatu kwa Kupunguza Msongamano wa Mahabusu Magereza

*Na Rebecca Kwandu*

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. George Masaju amepongeza taasisi zinazounda Utatu (Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, TAKUKURU na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya) kwa ushirikiano wao ambao umesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza msongamano wa Mahabusu magerezani.

*"Niwashukuru Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na timu yako kwa hatua hii mliyoifanya ya kuanzisha Utatu huu kwani kupitia umoja huo umesaidia kutatua changamoto mbalimbali tulizokuwa tunakumbana nazo magerezani ambazo kwa sasa zimepungua zikiwemo msongamano wa Mahabusu na wafungwa, ucheleweshwaji wa ukamilishwaji wa Upelelezi pamoja na ucheleweshwaji wa kusikilizwa kwa kesi ambazo ndizo zilikuwa changamoto na kasoro za mfumo wa Haki Jinai katika Taifa letu"*

Jaji Mkuu alibainisha hayo wakati akifungua Kikao kazi cha Menejimenti, Viongozi wa Mikoa na Wilaya wa Taasisi zinazounda Utatu kilichofanyika tarehe 19 Agosti, 2025 Jijini Dodoma.

Allifafanua kwa kusema *"Ukiangalia dira ya maendeleo ya mwaka 2050 imeweka kipaumbele kikubwa sana kwenye haki, mnavyofanya tathmini ya utendaji kazi wenu na kuweka mikakati mkumbukuke kuwa ninyi ni watu muhimu sana, lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi."*

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu alisema umoja na ushirikiano huo umewapa matokeo chanya kwa miaka minne ambayo wamekuwa wakishirikiana na kuleta mafanikio makubwa sana ikiwa ni pamoja na kuwa na ufanisi katika utendaji kazi wao ambao unaimarisha mifumo ya utoaji haki jinai nchini.

Aidha, Mkurugenzi wa Mashtaka alitoa shukrani kwa taasisi binafsi ya PAMS Foundation kwa kuwa wadau muhimu katika mapambano dhidi ya uhalifu.

*"Tunawashukuru wadau wote walioshiriki katika kikao kazi hiki na hii ni kwasababu ya umuhimu wa kikao hiki kwa kutambua kwamba wahalifu hawafungwi na mipaka lakini wanaweza kujificha na wakatenda uhalifu wao sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.''* Alisema Mkurugenzi Mwakitalu.

Naye, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Bw. Ramadhani Kingai alisema Kikao kazi hiki ni jukwaa muhimu la kuimarisha mshikamano katika taasisi zao katika mapambano dhidi ya uhalifu.

*"Uhalifu una sura nyingi na haupambaniwi kwa jitahada za taasisi moja tunapaswa kushirikiana sio tu kati ya taasisi zetu nne zinazounda Utatu bali pia na wadau wengine wote wa mnyororo wa Haki Jinai kama vile Mahakama, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhifadhi, Uhamiaji na wadau wengine kwani ushirikiano huo ndio unaojenga uimara wa taifa letu katika kudhibiti uhalifu na kuhakikisha haki inatendeka."*
Alisisitiza Mkurugenzi Kingai

Pia, Mkurugenzi wa Oparesheni na Mafunzo kutoka Shirika lisilo la kiserikali PAMS Foundation Bw. Samson Kassala alisema mashirikiano baina ya taasis za Haki Jinai ni sawa na viungo vya mwili ambavyo vinategemeana na kila kiungo kina sehemu ya kufanya kukamilisha mnyororo wote wa kuwasaidia wananchi waweze kuwa salama.



Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. George Masaju akihutubia kwenye ufunguzi wa Kikao kazi cha Menejimenti, Viongozi wa Mikoa na Wilaya wa Taasisi zinazounda Utatu kilichofanyika Jijini Dodoma.

# Mwanasheria Mkuu Anavyosimamia Upatikanaji Haki, Utekelezaji Dira 2050

*Na Leila Muhaji*



Moja ya nafasi ya juu ya uongozi na nyeti nchini ni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 59 (1).

Jukumu kubwa la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kuishauri Serikali katika masuala yote ya kisheria ndani na nje ya nchi katika maeneo ya Uandishi wa Sheria,Urekebu wa Sheria, Ufasiri Sheria, Upekuzi na Uchambuzi wa Mikataba mbalimbali ya kiuwekezaji.

Aidha, Ofisi hii inaiwakilisha Serikali kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala yenye maslahi kwa taifa kama yalivyooneshwa katika Ibara ya 59 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yanaainishwa katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268

Miongoni mwa majukumu hayo ni kuishauri Serikali kuhusu masuala yote ya Kisheria ikiwamo mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania ni sehemu ya mikataba ama ina maslahi katika mikataba hiyo.

Aidha, kutoa ushauri kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na taasisi za Serikali kuhusu mchakato wa utungwaji wa Sheria na masuala mengine yahusuyo Sheria, na kutoa ushauri stahiki wa Sheria zilizotungwa Sheria ndogo na maazimio mbalimbali na kuandaa miswada ya Sheria kwa ajili ya kuwasilishwa bungeni.

Majukumu mengine ni kuandaa hati zote za Kisheria na Maazimio kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge, Kushauri na Kudumisha Uhusiano kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kuleta ufanisi kuhusu suala lolote lililopo mahakamani na katika mabaraza.

Lingine ni kupokea taarifa kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka ili kushauri Serikali, Bunge na Mahakama.

Aidha, kuwasimamia Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali wote walioko katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika kutekeleza majukumu yao ya Kisheria, na kushiriki katika kudhibiti nidhamu ya Mawakili wa Kujitegemea kupitia Kamati ya Maadili ya Mawakili.

Katika kutekeleza haya, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya mambo mengi kuhakikisha majukumu yake yanaisaidia serikali katika eneo hili la Kisheria.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari anazungumzia namna Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilivyojipanga kwa miaka minne sasa ya Uongozi wa Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kutekeleza majukumu hayo kikamilifu.

Katika mahojiano na vyombo vya habari Ofisini kwake Jijini Dodoma, alibainisha ushiriki wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendesha Kliniki za Sheria katika Mikoa mbalimbali, kuandaa Juzuu ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali tangu mwaka 2002 na mafunzo ya Mawakili wa Serikali ili wawe na ubobezi katika kushughulikia mikataba mbalimbali inayoingiwa na Serikali.

Akizungumzia huduma za kliniki ya sheria na mchango wake katika kutatua changamoto za wananchi hususan wa kipato cha kawaida na cha chini katika upatikanaji wa haki, Mhe. Johari alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilibaini kuna changamoto kubwa kwa wananchi wa kawaida hasa walioko wilayani na mikoani katika kuzifikia huduma za kisheria.

Alisema wamekuwa wakihangaika na pia gharama za kupeleka mashauri mahakamani nazo ni kubwa, hivyo kuwa na umuhimu wa kuwasogelea wananchi katika mikoa na wilaya zao.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema, *"Kwa hiyo tulianzisha kamati za ushauri wa kisheria katika mikoa na wilaya. Baada ya kuanzisha tukaziwekea utaratibu au mwongozo wa kisheria wa mwaka 2024 unaolenga kuhakikisha tunasogeza huduma za kisheria hadi ngazi za wilaya na mikoa."*

Alisema moja ya nyenzo za utekelezaji wa mwongozo huo ilikuwa kuanzisha kliniki za huduma za kisheria, hasa kamati za ushauri za kisheria zinapoundwa, inaenda sambamba na wiki nzima ya utoaji wa huduma za kisheria kupitia kliniki, katika mkoa au wilaya ili kutoa huduma hizo bure.

Alisema, *"Tofauti na utaratibu mwingine wowote, tunapokuwa tunatoa huduma za kisheria kwa wananchi, mwananchi baada ya kuwasilisha shauri lake, lalamiko lake au jambo lake lolote linalohitaji msaada wa kisheria, tukishampa ule ushauri wa kisheria hauishii pale."*

Aliongeza *"Tunaendelea naye kumfuatilia kwa sababu tunaweka rekodi kwamba shauri hilo lilihusu nini, kama lilihusu ardhi, basi tunaliweka katika rekodi zetu, na kutoa ushauri na pia, kuendelea kulifuatilia hata baada ya pale hadi lifike mwisho na suala hilo la mwananchi kuwa limetatuliwa".*

Alisema, Kliniki hizo zinalenga kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi katika ngazi ya mikoa na wilaya. Tayari mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza imeshafikiwa, ambapo wananchi wamejitokeza kwa maelfu.

*"Lengo lilikuwa kusogeza huduma karibu na wananchi tukitimiza matakwa ya Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akisisitiza kusogeza huduma karibu na wananchi, lakini na kampeni ile ambayo inashabihiana na hii ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ya 'Samia Legal Aid Campaign,' lengo ni hilo la kusogeza huduma kwa wananchi,"* alieleza.

Akizungumzia lengo lingine la kuanzishwa kwa Kliniki za Sheria ni kuwapunguzia gharama wananchi. Alisema, *"Huduma hizi tunazitoa bure, kwa hiyo mwananchi anakuja anapata huduma na anaondoka".*

Alisema kuna shuhuda mmoja wa Mwanza alikuwa hajui pa kwenda na akifikiria gharama kubwa, alipofikiwa na huduma hizi aliona kama ni nyota ya jaha.

*"Kwa hiyo gharama zile tunawapunguzia kwa sababu wanakuja kupata huduma bure, na mawakili wa serikali tunawaweka pale, kwani huduma hizi zinatolewa na mawakili waandamizi wa serikali ambao ni wabobezi katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo wanapata huduma za kiwango cha juu bure".*

Lengo lingine kwa mujibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kuzipunguzia Mahakama mzigo wa Kesi nyingi ambazo alisema, si lazima zote ziende huko. *"Inawezekana nyingine tukakaa, tukazungumza, tukawasuluhisha watu na jambo likaisha".*

*"Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo unaipunguzia Mahakama mzigo mkubwa ilionao,"* alisema na kuongeza kuwa lengo lingine ni kuchagiza ukuaji wa shughuli za maendeleo na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

Alisema, lingine ni kusawazisha uhusiano kati ya waliokuwa kwenye migogoro hiyo ya kisheria au waliokuwa wanalalamikiana, ili wawe na amani na waishi katika amani kwa dhana ile ya haki wianishi.

Mhe. Johari alisema hadi sasa utekelezaji huo wa Kliniki za sheria umefikia wananchi 1,845 kwa mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza.

**"JUMLA YA WANANCHI**

**1,845**

***wamefikiwa na huduma za Kliniki ya Sheria bila malipo katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro na Mwanza."***

Ametaja kero kubwa zilizojitokeza ni Migogoro ya ardhi ambayo imebeba malalamiko 66.

*"Ardhi ni eneo ambalo kama Serikali inabidi tuweze kuliangalia vizuri kwa kushauriana na Wizara na Wadau wengine katika masuala ya ardhi ili kuona tunapunguzaje migogoro hiyo ya ardhi,"* alieleza Mwanasheria Mkuu.



Baadhi ya wananchi wakipata huduma za ushauri wa Kisheria kutoka kwa Mawakili wa Serikali wakati wa Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa mkoa wa Mwanza.

Aliyataja maeneo mengine kuwa ni ajira hasa katika sekta binafsi ambako waajiri wengi hawazingatii taratibu za kisheria katika masuala ya kazi na nguvu zaidi zinahitajika kupunguza kero hiyo.

Mengine yaliyolalamikiwa ni mirathi, ndoa na madai. Alisema ni jukumu la Serikali kuja na mbinu za kupunguza kero hizo zikiwamo Sheria na sera.

Akizungumzia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, hasa eneo la Kisheria, anasema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa maandalizi ya dira hiyo mpya na hata ile inayomalizika mwaka huu.

Alisema, "*Na pale itakapokuwa imepitishwa sasa na kuanza kutumika, basi na sisi tunaanza utekelezaji wa kuhakikisha kwamba kule tunakotaka kufika mwaka 2050, tunaweza kufika huko".*

Aliongeza, *"Kwa sababu kwenye Dira tunazungumza kwamba tunataka kuwa taifa ambalo litakuwa limepunguza umaskini kwa kiasi kikubwa na kuhakikisha uchumi wetu unakuwa na kufikia ngazi ya uchumi wa kati wa juu."*

*"Sasa lengo hilo ni kubwa, lakini tunaweza kufanikiwa kulifikia kama tu tutahakikisha kila mdau na kila mshiriki wa maendeleo na uchumi anachukua nafasi yake stahiki na kufanya yale ambayo yanapaswa kuhakikisha sisi tunafika huko tunakotarajia kufika mwaka 2050,"* alifafanua Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*"Baada ya kuisoma Dira ile kwa kina na kuielewa jambo la kwanza ambalo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutatakiwa kuhakikisha tunalitekeleza ni kuhakikisha tunaoanisha vizuri sheria tulizo nazo na kule tunakotaka kwenda,"* alieleza Mhe. Johari.

Aliongeza, *"Ili kufika tunakotaka kwenda, lazima kuwa na hiyo 'legal framework' (mpango wa kisheria) kutuwezesha kufika kule. Yaani sheria ni kama daraja la kutuvusha twende 2025 upande huu na 2050 upande ule, ni lazima tuwe na hilo daraja."*

Alisema kwa msingi huo, Sheria zote lazima zioane. "Tusipofanya hivyo, tutakuwa tunakwenda 2050, lakini Sheria zinavuta nyuma."

*"Ndio maana tunafanya marekebisho ya sheria; lengo ni hilo ni ili kunyumbulika na jamii inavyokwenda, unanyumbulika na sekta za kiuchumi zinavyokwenda, unanyumbulika na changamoto mbalimbali zinavyokwenda. Kwa hiyo katika dira hii zimedadavuliwa vizuri na jinsi zitakavyokwenda ili kufika 2050,"* alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kuhusu kutafsiri Sheria kwa Lugha ya Kiswahili, alisema kazi hiyo inaendelea na kati ya Julai hadi Desemba 2024, Sheria 300 zimeshatafsiriwa na ifikapo Juni 30, 2025 tutajua zimetafsiriwa ngapi.

Alisema kuanzia sasa sheria zitakuwa zinaandikwa kwa lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza ili kumrahisishia mtumiaji.

Tayari Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha Urekebu wa Sheria na sasa inaandaliwa Juzuu ya pamoja ya kuanzia Sheria zilizorekebishwa tangu mwaka 2002, ambazo sasa zitakuwa kwenye Juzuu moja zitazinduliwa hivi karibuni.

*"Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametimiza jambo kubwa ambalo kwa takribani miaka 22 tulikuwa hatujafanya urekebu wa sheria. Kwa mara ya mwisho Ilikuwa mwaka 2002... Safari hii tunalifanya tofauti kwa fedha zetu za ndani, huko nyuma hatukuwa na uwezo tulikuwa tunatumia fedha za wahisani,"* alisema.

Alimalizia kwa kusema, *"Tunapozungumzia Urekebu wa Sheria, tunazungumzia kujumuisha Marekebisho mbalimbali tunayofanya kila mwaka kwenye Juzuu moja ya Sheria ili kumrahisishia mtumiaji wa Sheria".*



Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wakipata huduma za ushauri wa masuala mbalimbali ya kisheria wakati wa Kliniki ya Sheria



Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu akimsikiliza Mwananchi wakati wa Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro.

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yawasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria

*Na Prisca Ulomi*



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akiwasilisha taarifa ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mbele ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria wakati wa kikao kilichofanyika Jijini Dodoma.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amesema kuwa Ofisi yake itaendelea kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi kwa weledi na ufanisi ili kuiwezesha Ofisi hiyokufikia malengo waliyojiwekea kwa wakati.

Dkt. Possi alisema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ikiwa ni sehemu ya utaratbu wa uwajibikaji na uwasilishaji wa taarifa za utendaji wa taasisi za Serikali katika kikao hicho kilichofanyika jijini Dodoma.

Dkt. Possi alieleza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa mhimili muhimu katika kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi jambo ambalo limeiwezesha Serikali kuepuka hasara kubwa na kuhakikisha haki inatendeka katika migogoro mbalimbali ya kisheria ndani na nje ya nchi.

Akiwasilisha taarifa yake, Dkt. Possi alisema kuwa, Ofisi yake imeimarisha usimamizi madhubuti wa mashauri yamadai kwa kusimamia na kushinda mashauri muhimu yaliyokuwa na athari kubwa kwa Serikali hivyo kuokoa fedha za umma ambazo zitaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo mathalani ujenzi wa miundombinu ya elimu, Vituo vya afya, miradi mikubwa ya barabara, viwanja vya ndege, bandari na reli ya kisasa ya SGR.

Pia, aliongeza kuwa Ofisi yake ilifanikiwa kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya usuluhishi wa migogoro kwa kutumia mbinu za kisheria na majadiliano, kumaliza migogoro mingi bila kufikia hatua ya mashitaka mahakamani hatua ambayo imeokoa muda na rasilimali za taifa.

Vile vile alisema kuwa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali katika kuhakikisha ushauri wa kisheria unazingatiwa kabla ya maamuzi makubwa kufanyika hivyo kupunguza uwezekano wa Serikali kuendelea kushitakiwa ndani na nje ya nchi.

Dkt. Possi alisema kuwa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikiali imeendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kuharakisha mchakato wa kushughulikia mashauri na kuendelea kuharakisha upatikanaji wa taarifa baina ya OWMS na wadau wake. Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Joseph Mhagama aliipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika tangu kuanzishwa kwake kwa kuendelea kusimamia mashauri kwa weledi na ufanisi na kuendelea kusaidia kuokoa fedha ambazo zitaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo.

Dkt. Mhagama alisisitiza kuwa Ofisi hiyo imeonyesha uwezo mkubwa wa kulinda maslahi ya taifa kupitia usimamizi bora wa mashauri ya madai na usuluhishi na kusisitiza umuhimu wa Ofisi kuendelea kujitangaza zaidi kwa umma ili wananchi wapate uelewa mpana kuhusu namna Ofisi hiyo inavyotekeleza majukumu yake katika kuendelea kulinda maslahi ya Taifa na mchango wake katika utawala wa sheria nchini.

"Ni muhimu Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kujitangaza zaidi kwa wananchi ili waelewe majukumu yake na namna inavyoshughulikia masuala ya kisheria yanayoihusu Serikali kwa kuwa wananchi wengi bado hawajui mchango wake katika kuhakikisha Serikali haipotezi rasilimali kupitia mashauri ya madai na usuluhishi," alisema Dkt. Mhagama.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo aliendelea kuhimiza Ofisi hii kuendelea kuimarisha mifumo yake ya utendaji ili kuboresha eneo la rasilimali watu na miundombinu katika kuhakikisha mashauri yote yanashughulikiwa kwa ufanisi zaidi.

Aidha, Dkt. Mhagama ameongeza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iendelee kuweka mikakati imara ya kushirikiana na taasisi za umma na binafsi katika kuhakikisha Serikali inalindwa kisheria ikiwa ni pamoja na kutumia vyombo vya habari na majukwaa mengine ya mawasiliano kutoa elimu kwa wananchi kuhusu majukumu ya Ofisi hii na namna wanavyoweza kunufaika nayo.



Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi, Alice Mtulo akifuatilia wasilisho la Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) kuhusu majukumu ya Ofisi ya Wakill Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Ofisi hiyo kilichofanyika Jijini Dodoma.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa kikao cha Kamati hiyo kilichofanyika Jijini Dodoma.




Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria wakifuatilia wasilisho la Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) kuhusu majukumu ya Ofisi hiyo wakati wa kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kilichofanyika Jijini Dodoma.

# " Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni Jeshi la Kulinda Nchi Dhidi ya Uhalifu wowote, Ndani na Nje ya Mipaka ya Nchi " - Dkt. Ndumbaro

*Na Rebecca Kwandu*



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi walioshiriki kwenye Hafla ya Makabidhiano ya magari ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ofisi za Wilaya iliyofanyika Jijini Dodoma.

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro amesema Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni jeshi la kulinda nchi dhidi ya uhalifu wowote, ndani na nje ya mipaka ya nchi na sifa kubwa ya Jeshi ni kushiriki mapigano ili kuiweka nchi na jamii kuwa salama.

*''Kazi yenu ninyi ni kuhakikisha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunakuwa na Haki, Amani, Usawa, na Maendeleo. Tukikosa haki na usawa tutakosa amani na nchi haitatawalika, kwa sababu wahalifu hawatakuwa na wasiwasi tena."*

Waziri Ndumbaro aliyasema hayo katika hafla ya kukabidhi magari 16 yaliyonunuliwa na Serikali kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya kutumika kwenye Ofisi za wilaya zake 16 iliyofanyika tarehe 15 Julai, 2025 katika Jengo jipya la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka lililopo Njedengwa, mtaa wa Mashtaka Jijini Dodoma.

Akizungumza katika hafla hiyo Mhe. Ndumbaro alisema kuwa magari yaliyokabidhiwa ni utekelezaji wa moja ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025 ya kupeleka huduma karibu na wananchi ikiwa ni pamoja na huduma za kimashtaka ambazo zinahitaji vitendea kazi kama magari.

*"Mhe. Rais ameweka fedha nyingi katika maboresho ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, tunaona jengo la ghorofa saba ambalo linakaribia kukamilika, magari mapya ya ziro kilomita na uwezeshaji unaofanyika katika ofisi za mikoa na wilaya, pia Mhe. Rais ameleta ajira nyingi katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashauri."* Alisema Dkt. Ndumbaro.

Pia aliwahimiza Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Madereva wanaokwenda kukabidhiwa magari hayo kuyatunza, kuyatumia na kuyaendesha kwa umakini kwani ni magari ya umma na hivyo yatumike kwa shughuli za umma na Serikali ili yarahisishe utekelezaji wa majukumu ya kila siku jambo litakalosaidia kupata vitendea kazi zaidi.

Aidha, Mhe. Ndumbaro aliipongeza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka chini ya Uongozi wa Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu na Menejimenti yake kwa kujenga timu imara inayofanya kazi vizuri na kupelekea malalamiko ya kesi kupungua.

Alisisitiza kuwa, kazi ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni kulinda nchi dhidi ya uhalifu, sio kuonea mtu bali kumfikisha mhalifu pale anapostahili, kwenda jela iwapo ana hatia au kuachiliwa huru iwapo hana hatia kupitia mhimili wa mahakama.

Sambamba na hilo, Waziri Ndumbaro ametoa wito kwa Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha nchi inakuwa na amani na usalama huku wakishughulika na ukatili wa kijinisia, utapeli katika masuala ya ardhi na kughushi nyaraka katika mambo ya mirathi ambayo ni masuala yaliyobainika katika Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia na kuihimiza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria kwa uhalifu utakaotendeka katika kipindi hiki cha uchaguzi kwani sheria haziendi likizo.

Naye Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Bi. Bibiana Kileo alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake kwa kuipatia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka magari ambayo ni vitendea kazi muhimu katika kutekeleza jukumu lake kuu la kuratibu upelelezi na uendeshaji wa Mashtaka.

Pia alieleza kuwa ugawaji wa magari hayo katika wilaya 16 zenye ofisi ya mashtaka umezingatia umbali na uhitaji wa kila wilaya ambapo magari hayo yatarahisisha utembeleaji wa vituo vya polisi na magereza kuwaona wazuiwa.

Aidha, magari hayo yamegawiwa katika wilaya za Momba, Kilosa, Gairo, Kilombero, Buhigwe, Iramba, Misenyi, Nyangh'wale, Ubungo, Kyera, Kilwa, Kaliua, Muleba, Uvinza na Kilolo ambayo yataongeza kasi ya utendaji kazi hususan uratibu wa upelelezi na uendeshaji wa mashtaka.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akimkabidhi Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo mfano wa funguo za magari ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyonunuliwa na Serikali.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akikata utepe kuashiria makabidhiano ya magari mapya ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika hafla ya kukabidhi magari yaliyonunuliwa na Serikali kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya kutumika kwenye Ofisi za wilaya zake 16 iliyofanyika katika jengo jipya la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka lililopo Njedengwa, mtaa wa Mashtaka Jijini Dodoma.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akiwakabidhi Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Madereva funguo za magari ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyonunuliwa na Serikali.

# Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na "Curtis Law Firm" Kushirikiana Kuwajengea Uwezo Mawakili

*— Na Leila Muhaji*



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno akizungumza wakati alipofanya kikao na Kampuni ya Kimataifa ya Mawakili ya Curtis (Curtis, Mallet-Pre-vost, Colt&Mosle LLP Law firm)

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno amefanya mazungumzo na Ujumbe kutoka Kampuni ya Kimataifa ya Mawakili ya Curtis (Curtis, Mallet-Prevost,Colt&Mosle LLP Law firm) kwa nia ya kuanzisha fursa za ushirikiano katika maeneo mbalimbali kati ya Kampuni hiyo na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Naibu Mwanasheria Mkuu alizungumza na ujumbe huo tarehe 30 Julai, 2025, ambapo alianza kwa kuwashukuru Kampuni ya Mawakili ya Curtis kwa utayari wao wa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika maeneo mbalimbali ya Sheria.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza kuwa kwa sasa Tanzania imekuwa ikitekeleza miradi mikubwa katika Sekta mbalimbali ikijumuisha Sekta ya Miundombinu, Uchukuzi, Nishati, Madini, Mawasiliano, Biashara na Uwekezaji.

Aidha, akizungumzia eneo la Uwekezaji, Mhe. Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alielezea dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kufungua fursa za Uwekezaji, hatua ambayo imeiwezesha Tanzania kuwa kituo bora cha Uwekezaji barani Afrika.

*"Nchi yetu kwa sasa inafunguka zaidi katika eneo la Uwekezaji, na hii inatokana na maboresho makubwa ya kisera , mazingira wezeshi ya Biashara na Ushirikiano mkubwa na sekta binafsi hususan katika sekta za kibiashara, nishati, miundombinu yanayoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, hivyo ninapenda kuwakaribisha kushirikiana nasi."* Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali .

Aidha, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisisitiza kuwa kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kuna umuhimu mkubwa kwa Mawakili wa Serikali kujengewa uwezo wa kitaaluma wa kimataifa katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na majadiliano, usimamizi wa mikataba, utatuzi wa migogoro na kushikishwa katika Kampuni kubwa za Uwakili duniani.

Akizungumza kwa niaba ya Kampuni ya Mawakili ya Curtis, Bi. Lise Johnson aliipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza ujuzi kwa Mawakili wa Serikali na kuahidi ushirikiano katika eneo hilo kulingana na uzoefu mkubwa walionao katika nyanja mbalimbali za Sheria.

Aidha, amezungumzia uzoefu walionao katika nyanja mbalimbali za Sheria ikiwa ni pamoja na maeneo ya Ushindani, uendeshaji wa mashauri, usuluhishi wa migogoro, uwekezaji na biashara, ulinzi wa taarifa, faragha na mtandao, Fedha, Hakimiliki, Dhamana na Mtaji, Kodi, majadiliano ya Mikataba, Mikataba ya Ujenzi, Nishati, Mafuta na Gesi, na Maktaba Mtandao( e- library).

Kampuni ya Curtis Law Firm ni Kampuni ya Kimataifa yenye Ofisi zake nchini Marekani, Amerika ya Kusini, Ulaya, na Mashariki ya Kati ikiwa na uzoefu wa muda mrefu katika maeneo ya Sheria na imekuwa ikishirikiana na nchi zinazoendelea kutoa msaada katika maeneo mbalimbali ikiwepo uendeshaji wa mashauri kwenye Mahakama za kimataifa pamoja na Mabaraza ya Usuluhishi ya Kimataifa (International Arbitration Tribunals).

Miongoni mwa nchi zinazoendelea ambazo Kampuni hiyo imefanya kazi nazo ni Uganda, Nigeria, Cameroon, Panama, Colombia na Argentina. Kikao hicho kilichoongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kilihudhuriwa pia na Mkurugenzi wa Mikataba na Makubaliano Bi. Sia Mrema, Wakili wa Serikali Mkuu Bi. Felista Lelo, Wakili wa Serikali Mkuu Bi. Catherine Paul na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Bi. Leila Muhaji.

# Wananchi Watakiwa Kupata Elimu ya Mpiga Kura Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

*Na Prisca Ulomi*




Wakili wa Serikali Mkuu, ndugu Deodatus Nyoni akizungumza na vyombo vya habari baada ya kusomwa kwa uamuzi wa Mahakama ulioruhusu Ofisi za TAMISEMI kuendelea kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini kwenye Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaiwakilisha Serikali kwenye shauri lililofunguliwa na Mahakama Kuu ya Tanzania, Masijala ndogo ya Dar es Salaam lililopinga Mamlaka ya Waziri wa TAMISEMI kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwezi Novemba, 2024.

Wakili wa Serikali Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Deodatus Nyoni akizungumza Mahakamani hapo baada ya kusikilizwa na kutolewa uamuzi kwa shauri la awali lililofunguliwa kwenye Mahakama hiyo, Masjala ndogo ya Dar es Salaam na wananchi watatu wakiongozwa na Bob Chacha Wangwe wakipinga Mamlaka ya Waziri wa TAMISEMI kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Serikali za Mitaa alisema kuwa Mawakili wa Ofisi hiyo walileta mapingamizi Mahakamani hapo ili kupinga matakwa ya waleta maombi.

Wakili Nyoni alieleza kuwa licha ya Mahakama kukubaliana na hoja za waleta maombi ambazo amezitaja kuwa ni pamoja na wahusika kuleta maombi yao ndani ya muda na kuwa na hoja za msingi lakini wao upande wa Serikali bado wanaamini mapingamizi yao yalikuwa na msingi na hivyo wanaheshimu maamuzi ya Mahakama hiyo kama yalivyotolewa na Mhe. Jaji Wilfredy Dyasobera.

Aliongeza kuwa pamoja na hoja zao kukubaliwa bado Mahakama imetupilia mbali aya nne zilizokuwa katika shauri hilo ambazo ni aya ya 10,15,17 na 19 kwa kuwa zilikuwa na shida na hivyo hazitakuwa sehemu ya nyaraka zitakazowasilishwa katika shauri la msingi kama waleta maombi wakiamua kufungua shauri husika.

Alieleza kuwa maombi haya ya kusimamisha uchaguzi kwa jinsi walivyokuwa wanayaomba hayakuwa sehemu ya maombi yao ya msingi hivyo ameendelea kuitaka Serikali kuendelea na taratibu zote inazoendelea kufanya ikiwa ni pamoja na kuendelea kuratibu zoezi la kuhamasisha wananchi ili ikifika muda mwafaka wananchi waweze kushiriki zoezi la uchaguzi wa Serikali za Mitaa na baadae mwakani washiriki zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Alihitimisha kwa kusema kuwa kwa kuwa upande wa waleta maombi wameelekezwa kuleta maombi yao mapema, Mawakili wa Serikali wako tayari kuyafanyia kazi kama vile yatavyokuwa yamekuja ili kuhakikisha haki inapatikana na uchaguzi uweze kufanyika kama ulivyopangwa katika kuhakikisha wananchi kote nchini wanapata haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua viongozi wanaowataka kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Mawakili wa Serikali wakiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, ndugu Deodatus Nyoni (wa kwanza kushoto) wakiwa na Mawakili wa Kujitegemea kabla ya kusikilizwa kwa uamuzi wa shauri la kupinga mamlaka ya Waziri wa TAMISEMI kutunga kanuni za kuratibu, kusimamia na kuendesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini uliosomwa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.



Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea wakiteta jambo kabla ya kusikilizwa kwa uamuzi wa shauri la kupinga mamlaka ya Waziri wa TAMISEMI kutunga kanuni za kuratibu, kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini uliosomwa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.

# Mafanikio ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita

*Na Rebecca Kwandu*

Baada ya kuingia madarakani Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alichukua hatua mahsusi ili kuiwezesha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kutekeleza majukumu ipasavyo mfano; Katika kipindi husika (Machi, 2021 hadi Septemba, 2025) OTM imewezeshwa kufungua Ofisi za Mashtaka katika Mikoa yote ya kijogorafia na mikoa ya Kimashtaka ambazo kwa pamoja ni 30 pamoja na Ofisi za Mashtaka katika Wilaya zipatazo 88.

Lengo la mpango huu ni kusogeza huduma za ki-mashtaka kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Hata hivyo kwa Wilaya 21 ambazo hazijafunguliwa ofisi za OTM zimefanyiwa tathmini tayari kwa kufunguliwa ofisi kulingana na upatikanaji wa rasilimali. Pia kwa sasa usimamizi wa Wilaya hizo unafanyika kwa ufanisi kwa Mawakili wa Serikali kutembelea kila wakati baada ya kuboreshwa kwa bajeti kutoka serikalini.

Kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya ununuaji, ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi. Mpaka sasa OTM imefanikiwa kutekeleza ujenzi wa jengo moja la Makao Makuu lilipo Dodoma na ujenzi wa Ofisi katika mikoa kumi na mbili (12) ya kimashtaka ambayo ni Ilala, Pwani, Morogoro, Mbeya, Manyara, Shinyanga, Geita, Njombe, Rukwa, Kinondoni, Temeke na Katavi ambapo ujenzi unaendelea katika hatua mbalimbali. Pia, ununuaji wa ofisi jengo la ofisi Mkoa wa Tanga pamoja na ukarabati wa jengo la ofisi Songea.

Katika kipindi husika Ofisi imewezeshwa kuajili Watumishi zaidi ambapo OTM imewezeshwa kuongeza watumishi kutoka watumishi jumla 630 Machi 2021 hadi kufikia watumishi Zaidi ya 1000 Septemba 2025 na hivyo kupunguza kwa sehemu changamoto ya upungufu wa rasilimali watu.

Bajeti ya OTM imeongezeka mwaka hadi mwaka ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka hivyo kuwezesha OTM kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. Hatua hii imepelekea kupunguza msongamano wa mahabusu Magerezani kutokana na kuimarika kwa usimamizi wa mashtaka na uratibu wa upelelekezi. Kwa upande mwingine hatua hii pia imepelekea kupungua kwa mrundikano wa mashauri Mahakamani kutokana na kuongozeka kwa ufanisi wa kazi kutokana na watumishi kujengewa uwezo kupitia mafunzo mambalimbali.

Maboresho katika ununuzi wa vitendea kazi kama magari, samani na vifaa vingine vya matumizi ya kawaida ya kuwezesha shughuli za ofisi ambavyo vimeleta hamasa na kurahisisha ufanyaji wa kazi.

Pamoja na hayo OTM imefanikiwa kuboresha mifumo ya usimamizi wa kesi na kuanzisha mfumo wa TEHAMA wa kusimamia kesi zinazowasilishwa OTM kwa hatua mbalimbali. Mfumo huu kwa kifupi unajulikana kama CMIS (Case Management Information System) umeboresha sana usimamizi wa kesi na kupunguza matumizi ya karatasi ambayo ni gharama. Katika kufanikisha suala hili OTM iliwezeshwa kununua vifaa vya TEHAMA ikiwemo komputa mpakato nakadharika.

Kutokana na kuongezewa bajeti na vitendea kazi na mafunzo kumepelekea kiwango cha kushinda kesi kuongezeka kutoka asilimia 45% Machi 2021 hadi kufikia 80% Septemba 2025 ambapo kwa sasa kuna mikakati kabambe ya kuongeza kiwango zaidi ya hapo.

Kuwekwa kwa mazingira mazuri yaliyopelekea Mkurugenzi wa Mashtaka kuweza kutoa miongozo mbalimbali ya usimamizi na uendeshaji wa mashtaka mahakamani. Kwa kipindi cha 2021 mpaka Septemba 2025 miongozo iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka ni pamoja na Miongozo inayohusiana na Ufunguaji mashtaka, Makubaliano ya Kukiri Makosa, Ulinzi wa Mashahidi, mashirikiano ya kimataifa na Utaifishaji Mali, Upelelezi na Uendeshaji wa Makosa Mtandao na Urejeshaji na Utaifishaji Mali.

Kwa kuhitimisha, OTM inaendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyokasimiwa kikatiba na sheria mbalimbali ikiwemo kuendesha mashtaka kwa weledi na kuhakikisha wananchi wanapata haki. Hii ni kwa mjibu wa moto wa taasisi ambao ni kutoa huduma bora za mashtaka kwa wakati na usawa kwa wote.



Jengo la Makao Makuu ya Ofisi yan Taifa ya Mashtaka.




Jengo la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Rukwa linalowakilisha Majengo yote ya Mikoa yanayojengwa.

# "Kitu cha Kwanza kwa Mwanasheria ni Kuhakikisha Kila Jambo Analifanya kwa Wakati na Ubora" - Mwanasheria Mkuu wa Serikali

*Na Leila Muhaji*

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari amewakumbusha Mawakili wa Serikali kufanya kazi kwa haraka, kwa wakati na kwa kuzingatia ubora, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameyasema hayo wakati akizungumza na Mawakili wa Serikali kwenye Mafunzo maalum kwa Mawakili hao yaliyofanyika tarehe 25 Machi, 2025 Jijini Arusha.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwakumbusha Mawakili wa Serikali kufanya kazi kwa haraka na kwa wakati ili waweze kuiishi kauli mbiu ya weledi na ubora pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi.

*"Ili tuifikie kauli mbiu yetu ya Weledi na Ubora ni lazima tuwe na tabia ya kufanya kazi kwa haraka na kwa wakati."* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*"Ili uwe Mwanasheria na mshauri mahiri ni lazima uyafahamu vizuri majukumu ya Serikali."* Alisema Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Katika hatua nyingine, Bw. Njole aliwakumbusha Mawakili wa Serikali kuzisoma na kuzielewa Sheria zinazosimamia Sekta mbalimbali ili waweze kuwa na wigo mpana wa utoaji wa ushauri kwa Serikali.

*"Kama Mwanasheria unatakiwa ufahamu mfumo wa kisheria wa sekta mbalimbali ili uweze kuwa mbobevu katika masuala ya kuishauri Serikali."* Alisema Bw. Njole



Aidha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alieleza kuwa mafunzo hayo kwa Mawakili wa Serikali yatasaidia kuongeza umahiri na kuwawezesha kutoa huduma bora za kisheria zitakazochangia katika kuleta maendeleo kwa Taifa.

*"Kuweza kutoa huduma bora za kisheria, kitu cha kwanza kwa Mwanasheria ni kuhakikisha kila jambo analifanya kwa wakati na kuzingatia ubora."* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Awali, akitoa mada kwa Mawakili wa Serikali Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole alieleza na kuwakumbusha Mawakili wa Serikali juu ya masuala muhimu ya kuzingatia wakati wanapoishauri Serikali ikiwemo kufahamu muundo na nyaraka mbalimbali za Serikali zitakazowasaidia kuelewa kwa kina majukumu na shughuli za Serikali.

Naye Jaji Mstaafu Mhe. Sirilius Matupa akichangia mada wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali, aliwakumbusha na kuwasisitiza kuhusu Weledi katika Uandishi na Uwasilishaji wa Ushauri wa Kisheria kwa Wadau, ambapo aliwasisitiza Mawakili hao kuwa mahiri katika nyanja mbalimbali za kisheria ili waweze kutoa ushauri utakaotatua changamoto zinazoweza kujitokeza.

*"Mawakili wanatakiwa kutoa ushauri kwa kufuata misingi ya kisheria na kuwasilisha ushauri wao kwa weledi ili ushauri wanaoutoa uweze kuwa na tija na kutatua changamoto husika."* Alisema Jaji Matupa

Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kufanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 24 hadi 28 Machi, 2025.




**Picha za Matukio mbalimbali wakati wa Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali katika Ukumbi wa AICC Jijini Arusha**








# Mahakama ya EAC Yatupilia Mbali Pingamizi la Bomba la Mafuta Uganda - Tanga

*Na Prisca Ulomi*



Mkurugenzi wa Idara ya Madai wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ndg. Mark Mulwambo akiwasilisha mapingamizi ya Serikali kwenye Shauri la Mradi wa Bomba la Mafuta lililosikilizwa kwenye Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Jijini Arusha.

Mnamo tarehe 29 Novemba, 2023, Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ilitoa uamuzi wake ambapo iilitupilia mbali pingamizi dhidi ya mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki linalojengwa kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania. Uamuzi huu unatokana na shauri la maombi Namba. 29 la mwaka 2020 lililofunguliwa na Center for Food and Adequate Living Rights Limited na wenzake watatu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Uganda na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Katika madai yao, Walalamikaji walidai kwamba Mkataba wa utekelezaji wa Mradi huo wa Bomba la Mafuta unakiuka misingi ya haki za binadamu na utasababisha uharibifu wa mazingira kinyume na Ibara ya 6(2)(d), 7(2) na 8(1)(c) ya Mkataba wa Kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Mkataba wa Usimamizi wa Ziwa Victoria chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Walalamikaji walifungua shauri dogo la maombi ya kuzuia utekelezaji wa mradi huo katika Mahakama hii.

Katika utetezi wake, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilibainisha kwamba Mkataba huo wa utekelezaji wa Bomba la Mafuta umezingatia misingi yote ya haki za binadamu ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kina kuhusu athari za mazingira na haki za binadamu zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake na kwamba hakuna athari zozote zilizobainikwa kufanya mradi kuwa kinyume na Mkataba wa uanzishwaii wa Jumuiva ya Afrika Mashariki pamoja na Mkataba wa Usimamizi wa Ziwa Victoria. Hivyo, athari ndogo zilizobainishwa kwenye utafiti uliofanywa ziliwekewa mipango mathubuti ya kuweza kuthibiti athari zake kwa mazingira na haki za binadamu.

Sambamba na utetezi huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo iliwakilishwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, iliwasilisha mapingamizi matatu (3) ya kisheria kuhoji mamlaka ya Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuweza kusikiliza shauri hilo. Msingi wa hoja za kisheria ulitokana na kwamba Mkataba unaolalamikiwa kati ya Tanzania na Uganda ulisainiwa tarehe 26 Mei, 2017 na wakati Ibara ya 30(2) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inataka malalamiko kuhusu jambo lolote dhidi ya nchi mwanachama wa Jumuiya kuwasilishwa Mahakamani ndani ya siku sitini (60) tangu kufanyika kwa jambo husika. Hoja hii pia iliungwa mkono na Serikali ya Uganda pamoja na hoja nyingine zilizohusu hati ya madai kutokuthibishwa na Walalamikaji na mamlaka ya

Mahakama kusikiliza masuala yanayohusu haki za binadamu.

## UAMUZI WA MAHAKAMA

Katika uamuzi wake, Mahakama imekubaliana na hoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba Mahakama haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kwa kuwa linahusu madai ambayo yalitakiwa kuwasilishwa ndani ya muda wa siku sitini (60) kwa mujibu wa Ibara ya 30(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, Mkataba unaolalamikiwa, ulingiwa tarehe 26 Mei, 2017 kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda.

Mahakama pia imebaini kwamba walalamikaji walikuwa na taarifa hiyo na hawakuchukua hatua zozote za kisheria mpaka walivyofanya hivyo Novemba, 2020 ambayo ilikuwa ni zaidi ya miaka mitatu (3) tangu kuingiwa kwa Mkataba huo. Hivyo, baada ya kujiridhisha kwamba malalamiko hayo yanakiuka matakwa ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama imeyatupilia mbali malalamiko hayo pamoja na shauri husika kwa gharama (dismissed with costs).

## HITIMISHO

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatoa shukrani za dhati kwa taasisi zote za Serikali na wadau wengine ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Uganda na Ofisi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ushirikiano wao katika uendeshaji wa shauri hili. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendelea kufanya kazi kwa weledi, uaminifu na uadilifu katika kutelekeza majukumu yake ya ushauri, uratibu na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali na Taasisi zake ndani na nje ya nchi.




Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa na Mawakili wa kujitegemea baada ya kusikiliza shauri kwa ajili ya kupanga mwenendo wa uendeshaji wa rufaa ya shauri lililofunguliwa na Halmashauri ya Kijiji cha Ololosokwan na vijiji vingine vitatu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki Jijini Arusha.

# Mashirikiano Kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na UNODC Yazidi Kuimarika katika Kutokomeza Kesi za Ukatili wa Kijinsia

*Na Rebecca Kwandu*




Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akifungua mafunzo juu ya namna ya ushughulikiaji wa Makosa ya Ukatili wa Kijinsia kwa Mawakili wa Serikali ambao ni baadhi ya Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi 50 yaliyofanyika katika Hotel ya Four Points by Sheraton Jijini Dar es salaam

Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu amefungua mafunzo juu ya namna ya Ushughulikiaji wa Makosa ya Ukatili wa Kijinsia kwa Mawakili wa Serikali ambao ni baadhi ya Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi 50 yaliyofanyika kuanzia tarehe 2 hadi 4 Septemba, 2025 katika Hotel ya Four Points by Sheraton Jijini Dar es salaam.

Mafunzo hayo maalum kwa Waendesha Mashtaka yaliandaliwa na Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa lengo la kuwajengea uwezo washiriki hao katika kupambana na kesi za Ukatili wa kijnsia.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo Mkurugenzi wa Mashtaka alitoa shukrani kwa UNODC kwa kufadhili na kusaidia kufanikisha mafunzo haya muhimu ambayo yanaakisi dhamira ya kujenga jamii yenye usawa kwa raia wote, hususan kwa wanawake na watoto.

Pia alimshukuru Bi. Linda Naidoo ambae ni Mratibu wa UNODC kwenye masuala ya Ukatili wa Kjinsia kutoka ofisi za SADC pamoja na timu yake nzima kwa kuratibu mafunzo haya muhimu.

*"Kama Ofisi ya Taifa ya Mashtaka tuna ufahamu mzuri kwamba mapambano dhidi ya Ukatili wa kijinsia yanahitaji jibu thabiti la haki linalomzingatia manusura. Hii si tu kuhusu kuwafikisha wahalifu mahakamani bali pia kurejesha heshima, kulinda manusura, na kutuma ujumbe wazi kwamba Ukatili wa Kijinsia hauna nafasi katika jamii yetu."* Alisema Mkurugenzi Mwakitalu.

Alieleza pia Ufanisi wa Mashtaka kuhusu mashauri ya unyanyasaji wa kijinsia unahitaji

ushirikiano mzuri baina ya Waendesha Mashtaka, Polisi, Wafanyakazi wa Afya, Maafisa wa Ustawi wa Jamii, na Viongozi wa Kijamii. Tumekusudia kukuza njia ya ushirikiano ambapo taarifa zinashughulikiwa kwa ufanisi, wahanga wanapata msaada wa kina, na wahalifu wanawajibishwa kikamilifu.

Aidha, aliwahimiza washiriki hao kutumia fursa hii si tu kuboresha ujuzi bali pia kuimarisha dhamira haki, usawa, na utu.

Kwa upande wake, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo aliwaasa washiriki wa mafunzo haya kuwa wamepata nafsi adimu sana hivyo waitumie kuhakikisha wanapata uelewa ambao utaleta tija kwa taasisi na wadau wengine. Mwisho alimkaribisha Mkurugenzi wa Mashtaka kuweza kufungua kikao.

Naye, Mratibu wa UNODC kwenye masuala ya Ukatili wa Kijinsia kutoka Ofisi za SADC Bi. Linda Naidoo aliipongeza Ofisi ya Taifa ya Taifa ya Mashtaka akiongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu kwa juhudi wanazozitoa katika kupambana na kesi za Ukatili wa Kijinsia hususan kwa wanawake na watoto hivyo aliwataka kutokukata tamaa na zaidi kuendelea kukuza mashirikiano baina yao ili kuweza kutokomeza ukatili huo kwani unaleta huzuni na kurudisha maendeleo ya kiuchumi katika jamii kwa ujumla.




Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa mafunzo juu ya namna ya ushughulikiaji wa Makosa ya Ukatili wa Kijinsia kwa Mawakili wa Serikali ambao ni baadhi ya Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi 50 yaliyofanyika katika Hotel ya Four Points by Sheraton Jijini Dar es salaam



# Kamati ya Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo Yazinduliwa Singida

- *"Tutatoa huduma hii bure na kwa weledi mkubwa" – Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

*Na Leila Muhaji*

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida imezindua rasmi Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria bila malipo kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida. Uzinduzi huo umefanyika tarehe 19 Mei, 2025 katika Viwanja vya Stendi ya Zamani, Manispaa ya Singida.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mgeni Rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima O. Dendego aliipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuuchagua Mkoa wa Singida na kuja kuzindua Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa kuwa ni fursa kwa wananchi wa mkoa huo kutatuliwa changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili.

*"Kipekee naishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa kunifikiria na kunipa wajibu huu mkubwa wa kuwa Mgeni Rasmi katika Halfa hii ya Uzinduzi wa Kamati na Kliniki ya Sheria bila malipo katika mkoa wetu".* Alisema Mhe. Dendego.

Mhe. Dendego alisema kuwa kuzinduliwa kwa Kamati hiyo pamoja na masuala mengine, kutasaidia Kupunguza mashauri au migogoro dhidi ya Serikali, kuwawezesha Mawakili wa Serikali kusimamia Utawala wa Sheria katika maeneo yao, Kuwawezesha Mawakili wa Serikali kushirikiana na wadau wengine katika kutatua kero za wananchi na kupunguza malalamiko ya kisheria kutoka kwa wananchi.

*"Naomba kukuahidi Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa nitazisimamia Kamati hizi kikamilifu ili ziweze kuwa na tija katika mkoa wetu."* Alisema Mhe. Dendego

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Singida alitoa wito kwa Wananchi wa Mkoa huo kujitokeza kwa wingi katika Kliniki ya Sheria bila malipo ili waweze kupata huduma mbalimbali za kisheria hususan katika masuala ya mirathi, Ardhi, ndoa na Ajira.

*"Nitoe wito kwa Wananchi wa Singida kujitokeza kwa wingi katika Kliniki hii kwani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuja na Wataalamu waliobobea katika masuala ya Kisheria na wanatoa huduma hii bure kabisa."* Alisema Mhe. Dendego.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari alisema kuwa kuzinduliwa kwa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na Kliniki ya Sheria kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida ni mojawapo

ya hatua za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kusogeza huduma za kisheria karibu zaidi na wananchi.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza kuwa moja ya njia inayotumiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwajibika kwa wananchi ni kutoa ushauri na msaada wa kisheria kwa kutumia Kamati za Ushauri wa Kisheria kwa ngazi ya Mkoa na ngazi za Wilaya.

*"Lengo kuu la uanzishwaji wa Kamati za Ushauri wa Kisheria kwa ngazi ya Mkoa na Wilaya ni kurahisisha usimamizi wa utoaji wa ushauri wa kisheria kwa wananchi katika maeneo husika".* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa, Uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria kwa Mkoa wa Singida utafuatiwa na Kliniki ya Sheria, ambapo huduma za ushauri wa kisheria zitatolewa kwa wananchi bila malipo na alisisitiza kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itatoa huduma hizo kwa ubora.

*"Tunawaahidi tutatoa huduma hii bila malipo kwa wananchi na kwa weledi mkubwa".* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Vilevile, Mhe. Johari alisema kuwa Kliniki hiyo ya Sheria inalenga kusogeza huduma za sheria karibu na wananchi, kuwaongoza wananchi katika taratibu za kupata haki zao pale zinapovunjwa au zinapoonekana kuelekea kuvunjwa, kutoa elimu ya sheria kwa wananchi na kuongeza ushirikiano miongoni mwa Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea, na kuepusha au kupunguza mashauri yasiyo ya lazima.

*"Kupitia huduma zitakazotolewa kwenye Kliniki hii ya Sheria tunaamini tutaongeza utengamano na utulivu katika jamii, kudumisha utawala bora kwa kuimarisha utawala wa sheria nchini, na kuchochea maendeleo kwa jamii na taifa kwa ujumla".* Alisema Mhe. Johari.

Kliniki ya Sheria bila malipo kwa Mkoa wa Singida, ilizinduliwa tarehe 19 Mei na kuendelea kutoa huduma za kisheria kwa wananchi wa mkoa wa Singida hadi tarehe 25 Mei, 2025 katika Viwanja vya Stendi ya Zamani, Manispaa ya Singida.



Baadhi ya Wananchi wakipata huduma ya ushauri wa kisheria kutoka kwa Mawakili wa Serikali wakati wa Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa mkoa wa Singida, iliyofanyika katika Viwanja vya Stendi ya Zamani, Manispaa ya Singida.

# Mahakama Yatoa Uamuzi Kuhusu Uhalali wa Uwepo wa Pori la Akiba la Pololeti, Wilaya ya Ngorongoro, Arusha

*—— Na Prisca Ulomi ——*




Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa na Mawakili wa kujitegemea baada ya kusikiliza shauri kwa ajili ya kupanga mwenendo wa uendeshaji wa rufaa ya shauri lililofunguliwa na Halmashauri ya Kijiji cha Ololosokwan na vijiji vingine vitatu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki Jijini Arusha.

Mnamo tarehe 19 Septemba, 2023; Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha mbele ya Mhe. Jaji J.C. Tiganga ilitoa uamuzi katika shauri Namba 21 la Mwaka 2022 baina ya Ndalamia Partareto Taiwap na wenzake wanne dhidi ya Waziri wa Maliasili na Utalii na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Waleta maombi katika Shauri hili ni wananchi wakazi wa Tarafa za Loliondo na Sale, Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha. Kiini cha mgogoro huu ni madai ya wananchi hao kuondolewa katika eneo lililokuwa Pori Tengefu la Pololeti (Pololeti Game Controlled Area) lililoanzishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 421 la tarehe 17 Juni 2022 (Wildlife Conservation (Pololeti Controlled Area) (Declaration Order), 2022) lilitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Wananchi hao wanadai kuwa walikuwa wamiliki halali wa eneo husika kabla ya kutangazwa kuwa Pori Tengefu mwaka 2022.

Mashauri hayo yalitolewa maamuzi na Mahakama Kuu ya Tanzania. Maamuzi haya ya Mahakama katika shauri Namba 21 la Mwaka 2022 yakisomwa kwa pamoja na maamuzi katika maombi Na 178 ya Mwaka 2022 yana maana ifuatayo:-

(i) Tangazo Na.421 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori Tengefu la Pololeti halipo tena katika macho ya sheria kwa kuwa tayari Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelipandisha hadhi eneo hilo kuwa Pori la Akiba;

(ii) Mahakama imesitisha utekelezai Tamko la Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupitia Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori la Akiba la Pololeti mpaka usikilizwaji wa kesi ya msingi Na. 18 ya Mwaka 2023 utakapo kamilika;

(iii) Usitishwaji wa utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022, unawahusu waleta maombi katika shauri Na. 178 la Mwaka 2022 na haiwahusu watu wengine;

(iv) Kwa kuwa Tangazo Na. 421 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori Tengefu la Pololeti halipo tena na Mahakama imesitisha utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori la Akiba la Pololeti, hali ilivyo kwa sasa (status quo) wakati ukisubiriwa namuzi wa Mahakama katika kesi ya msingi Na. 18 ya Mwaka 2023 ni kwamba eneo lenye mgogoro linaendelea kuwa Pori Tengefu hali iliyokuwa nayo kabla ya kupandishwa hadhi kuwa Pori la Akiba mpaka Mahakama itakapotoanamuzi kwenye Shauri la msingi. Kwa msingi huomasharti vote vanayosimamia mapori tengefu

yanafuatwa ikiwemo kuomba kibali kwa Mkurugenzi wa Wanyapori ili kulisha mifugo katika eneo la Pori Tengefu kwa mujibu wa kifungu cha 21 cha Sheria ya Wanyama Pori, Sura ya 283 Juzuu la Marejeo ya 2022.

(v) Wananchi na wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii wanakumbushwa kuzingatia sheria katika utekelezaji wa shughuli zao.

Aidha, mnamo tarehe 14 Oktoba, 2022, Pori hilo la Pololeti lilipandishwa hadhi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Pori la Akiba yaani Wildlife Conservation (Pololeti Game Reserve) (Declaration) Order, 2022 kupitia Tangazo la Serikali Na. 604 la 2022.

Katika maombi yao Mahakamani, waleta maombi waliomba Mahakama itoe amri ya kumzuia Waziri wa Maliasili na Utalii kuwaondoa waleta maombi na wakazi wa vijiji 14 kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500 zinazotengeneza Pori la Akiba la Pololeti.

Ikumbukwe kuwa, tarehe 22 Agosti, 2023; Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha mbele ya Mhe. Jaji D. C. Kamuzora ilitoa uamuzi wake katika maombi Na. 178 ya Mwaka 2022 yaliyofunguliwa na Latan'gamwaki Ndwati na wenzake 6 wakiomba Mahakama itoe idhini (leave) ya kufungua shauri la kupinga Tamko la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuanzisha Pori la Akiba Pololeti, 2022 (Pololeti Game Reserve Declaration Order) G.N No. 604 of 2022. Mahakama katika uamuzi wake iliamua yafuatayo:-

i. Ilitoa idhini (leave) kwa waleta maombi kufungua shauri la kupinga utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022; na

ii. Ilisitisha utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 mpaka usikilizwaji wa kesi ya msingi utakapo kamilika.

Wadai walifungua maombi ya marejeo ya Kimahakama (judicial review) Na. 18 ya Mwaka 2023 katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha ambayo yalisikilizwa na kutolewa maamuzi.

Katika uamuzi wake, Mahakama imetupilia maombi hayo ya waleta maombi na kubainisha kwamba Tangazo Na.421 la mwaka 2022 lililotolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii halipo tena katika macho ya sheria kwa kuwa tayari Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelipandisha hadhi eneo hilo kuwa Pori la Akiba (Game Reserve, GR), kupitia Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 na hivyo hakutakuwa na maamuzi yatakayokuwa na nguvu dhidi ya tangazo hilo kwa kuwa halipo tena.

Aidha, Mahakama katika uchambuzi wa hoja zilizokuwa mbele yake ilibaini kwamba eneo ambapo Pori hilo lipo lilikuwepo tangu mwaka 1951. Hivyo, Vijiji viliposajiliwa vililikuta tayari limeanzishwa kama Pori Tengefu ambalo lilijulikana kama Loliondo Game Controlled Area na hoja kwamba eneo hilo ni ardhi ya kijiji moja kwa moja (exclusive) sio kweli bali vijiji ndivyo vilikuta Pori hilo Tengefu. Hoja nyingine tisa (9) za waleta maombi zilitupiliwa mbali na Mahakama kwa kuwa hazikuwa na mashiko kisheria.




Rais wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mhe. Jaji Nestory Kayobera (aliyeketi nyuma katikati) akiwa mahakamani wakati wa Kongamano la Awali kwa ajili ya kupanga mwenendo wa usikilizaji wa rufaa iliyofunguliwa na Halmashauri ya Kijiji cha Ololosokwan na vijiji vingine vitatu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mahakama hiyo Jijini Arusha.

# DPP Akabidhiwa Juzuu za Toleo la Urekebu wa Sheria la Mwaka 2023

*Na Rebecca Kwandu*




Mkurugenzi wa Mashitaka Bw. Sylvester Mwakitalu akiwa katika picha ya pamoja na baadhi menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na timu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali



Mkurugenzi wa Mashitaka Bw. Sylvester Mwakitalu akizungumza na timu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka mara baada ya kuwasili katika Ofisi yake Mkao Makuu Jijini Dodoma kwa lengo la kumkabidhi Juzuu za toleo la Urekebu wa Sheria la mwaka 2023 pamoja na tuzo maalumu ya heshima.



Mkurugenzi wa Mashitaka Bw. Sylvester Mwakitalu akipokea Juzuu za toleo la Urekebu wa Sheria la mwaka 2023 kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Divisheni ya Urekebu, Tafiti na Mafunzo, Bi. Rehema Katuga, kwa niaba ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Tuzo hiyo imetolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnamo tarehe 12 Septemba, 2025 Makao Makuu Jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Mashitaka Bw. Sylvester Mwakitalu amepokea Juzuu za toleo la Urekebu wa Sheria la mwaka 2023 pamoja na tuzo maalum ya heshima kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Divisheni ya Urekebu, Tafiti na Mafunzo, Bi. Rehema Katuga, kwa niaba ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Tuzo hiyo imetolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnamo tarehe 12 Septemba, 2025 Makao Makuu Jijini Dodoma ikiwa ni ishara ya kutambua mchango mkubwa wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kufanikisha zoezi hilo la kihistoria.

Toleo la Urekebu wa Sheria la mwaka 2023 lilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, mnamo mwezi Aprili, 2025 na lilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2025, hivyo kufuta toleo lililotumika tangu mwaka 2002.

Akizungumza mara baada ya makabidhiano hayo Mkurugenzi wa Mashtaka aliipongeza Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kazi kubwa kufanikisha Urekebu huo na kuahidi kusambaza Nakala zilizopokelewa kwa Mawakili wa Serikali.

Aidha, alibainisha kuwa Sheria hizo ni nyenzo muhimu kwa kazi za mashitaka zinazofanyika kila siku katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Divisheni ya Urekebu, Tafiti na Mafunzo, Bi. Rehema Katuga alieleza kuwa ushirikiano wa karibu kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, hususan kupitia Mawakili walioungana nao wakati wa changamoto za uhaba wa watumishi, ulikuwa chachu ya kukamilisha kazi hiyo. Pia aliongeza kuwa Nakala zote za toleo hilo zinapatikana kupitia mfumo wa OAG MIS Library kwa matumizi ya kila siku.

# Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kuboresha Sheria Kuelekea Utekelezaji wa Dira 2050

*Na Leila Muhaji*



Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari akitoa hotuba ya ufunguzi wa kikao cha Baraza la wafanyakazi, kilichofanyika Jijini Dodoma.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanza kufanya maboresho ya Sheria mbalimbali ili kurahisisha utekelezaji wa Dira 2050.

Hayo yalisemwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari wakati wa Kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kilichofanyika tarehe 18 Agosti, 2025 Jijini Dodoma.

Akizungumza wakati wa Ufunguzi wa Kikao cha Baraza la Wafanyakazi, Mhe. Hamza S. Johari ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanza mkakati wa kufanya maboresho katika sheria ili kuhakikisha kuwa, sheria, sera, mipango, malengo na mikakati mbalimbali pamoja na vigezo na viashiria vilivyowekwa vya upimaji wa matokeo ya kiutendaji wa Watumishi wa umma, vinafungamanishwa na malengo na shabaha ya Dira ya 2050.

*"Ofisi yetu, inao wajibu wa kupanga, kuratibu, kutekeleza michakato ya tathmini na mapitio ya sheria za Bunge na sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kufanya maboresho na marekebisho muhimu ili kuziwezesha Taasisi za Umma kushiriki kikamilifu katika Utekelezaji wa Dira ya 2050 kwa ufanisi na tija."* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwaeleza Wajumbe wa Baraza kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kutekeleza mpango kazi wake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa kuandaa Miswada mbalimbali ya Sheria 19, kutafsiri Sheria Kuu 433 kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili, kuandaa maazimio mawili ambayo yaliidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kukamilisha Urekebu wa Sheria Kuu 446 za nchi na kuandaa Toleo la Sheria zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2023.

Vilevile, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa jumla ya Mikataba 3,436 ya Kitaifa na Kimataifa na Hati za Makubaliano (Memorandum of Understanding) 729 zilifanyiwa upekuzi na takribani maombi 4,151 ya ushauri wa kisheria yalipokelewa na kufanyiwa kazi.

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwakumbusha Wajumbe wa Baraza na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na misingi mikuu minne ambayo ni Utaalamu/Weledi, Ubunifu, Uadilifu na Uwazi, ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Dira na Dhima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*"Maafisa na Watumishi wote tulio hapa, ni jukumu letu kuhakikisha Dhima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatekelezwa ili kufikia Dira ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali."*

Awali, akimkaribisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno alisema kuwa Baraza hilo limekutana kwa lengo la kupitia mipango mbalimbali iliyotekelezwa, inayotekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*"Mhe. Mwenyekiti leo tumekutana kwa ajili ya kupitia mipango tuliyoiweka kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ili iweze kushauriwa na pengine kupewa maelekezo mbalimbali ambayo ni muhimu kuzingatiwa, ikihusisha masuala yanayohusu Wafanyakazi na utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali."* Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TUGHE tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Zella Rwemanyila aliushukuru Uongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*"Chama cha Wafanyakazi TUGHE tunawapongeza viongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa jitihada zenu mnazozifanya na mnazoendelea kuzifanya katika kuhakikisha kuwa mnaboresha mazingira ya kazi katika Ofisi yetu."* Alisema Bi. Zella.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa TUGHE tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bi. Zella Rwemanyila akiwasilisha hoja za Wafanyakazi wakati wa ufunguzi wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Jijini Dodoma.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari (katikati walioketi), akiwa katika picha ya pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno (wa tatu kutoka kulia walioketi) Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole (wa pili kushoto walioketi) na baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baadhi ya Viongozi wa TUGHE mara baada ya ufunguzi wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Jijini Dodoma.

# Rufaa Inayopinga Ujenzi wa Bomba la Mafuta Yatupiliwa Mbali

*Na Prisca Ulomi*

Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameiomba Divisheni ya Rufaa ya Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACJ) kutupilia mbali rufaa inayopinga ujenzi wa bomba la mafuta linalojengwa kutoka Hoima, Uganda kuja Tanga, Tanzania lililofunguliwa na Center for Food and Adequate Living Rights (CEFROHT) Limited na wenzake watatu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Uganda, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Jopo la Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu na Mkurugenzi wa Idara ya Madai wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali . Ndugu Mark Mulwambo wameiomba Mahakama kutupilia mbali rufaa inayopinga ujenzi wa bomba la mafuta linalojengwa kutoka Hoima, Uganda kuja Tanga, Tanzania kwa kubaini ukosefu wa nyaraka za mwenendo wa shauri hilo lililofanyika Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Divisheni ya Awali.

Wakili wa Serikali Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Mulwambo ameiomba Mahakama kutupilia mbali rufaa hiyo kwa mujibu wa Kanuni za Uendeshaji Mashauri kwenye Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kanuni ya 98(1)(h).

Mawakili wa wakata rufaa wakiongozwa na Wakili wa Kujitegemea, Justin Semuyaba walikubali kuwa rufaa yao ina mapungufu hivyo wameiomba Mahakama iwapemuda wa wiki mbili ili walete nyaraka zilizopungua.

Jopo la Majaji watano wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACJ) wakiongozwa na Rais wa Mahakama hiyo, Mhe. Jaji Nestory Kayobera baada ya kusikiliza ombi la Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania wamesitisha usikilizaji wa rufaa hiyo iliyopangwa kufanyika leo Mahakamani hapo na kuelekeza warufani wawasilishe nyaraka za mwenendo wa shauri hilo lililoamuliwa kwenye Divisheni ya Awali ya Mahakama ya EACJ ifikapo tarehe 29 Novemba, 2024 ili Divisheni ya Rufaa ya Mahakama ya EACJ iweze kupanga tena tarehe ya kusikilizwa kwa shauri hilo.





Mawakili wa Serikali ya Tanzania na Uganda wakiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Madai wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mark Mulwambo (wa tatu kushoto) na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ya Uganda, Charles Ouma (wa nne kulia) wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kumaliza kusikiliza rufaa inayopinga ujenzi wa bomba la mafuta kwenye Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Jijini Arusha.



Rais wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Mhe. Jaji Nestory Kayobera (aliyeketi Katikati) akiongoza jopo la majaji watano wa Mahakama hiyo kusikiliza rufaa inayopinga ujenzi wa bomba la mafuta kwenye Mahakama hiyo Jijini Arusha.



Baadhi ya wananchi wakiwa kwenye ukumbi wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wakisikiliza rufaa ya kupinga ujenzi wa bomba la mafuta linalojengwa kutoka Hoima, Uganda kuja Tanga, Tanzania kwenye Mahakama hiyo Jijini Arusha.



Mkurugenzi wa Idara ya Madai wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo akiwasilisha mapingamizi ya Serikali kwenye rufaa inayopinga ujenzi wa bomba la mafuta linalojengwa kutoka Hoima, Uganda kuja Tanga, Tanzania kwenye Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Jijini Arusha.

# Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Azitaka Kamati za Ujenzi Wilayani Kusimamia Kikamilifu Miradi ya Ujenzi

*—— Na Rebecca Kwandu ——*



Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Kikao kazi na Mafunzo ya namna bora yakutekeleza miradi ya ujenzi kwa kutumia Mfumo wa matumizi ya rasilimali za ndani (Force Account) kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Wilaya yaliyofanyika tarehe 7 Desemba, 2024.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo amewataka wajumbe wa Kamati za Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi pamoja na Kamati za Ukaguzi na Mapokezi kuhakikisha zinasimamia kikamilifu miradi ya ujenzi ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kutumia vizuri Mfumo wa Matumizi ya Rasilimali za Ndani (Force Account) ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, alibainisha hayo wakati akifungua kikao kazi na mafunzo ya namna bora ya kutekeleza miradi ya ujenzi kwa kutumia Mfumo wa Matumizi ya Rasilimali za Ndani (Force Account) kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Wilaya kilichofanyika katika ofisi za mashtaka jijini Dodoma.

Kikao hicho kilihusisha wajumbe wa Kamati za Ujenzi na Kamati za Ukaguzi na Mapokezi kutoka Wilaya 24, Kamati ya Uratibu wa Ujenzi Makao Makuu, Washiriki kutoka baadhi ya Divisheni na Vitengo pamoja na wataalamu kutoka Wakala wa Ununuzi wa Umma (PPRA) pamoja na Wizara ya Fedha.

Kikao kazi cha Kamati za Ujenzi kililenga katika kujadiliana, kupata mafunzo na miongozo ya namna bora ya kusimamia miradi ya ujenzi wa Ofisi za Mikoa mitatu (3) na Wilaya 24 ambayo Ofisi ilikuwa katika mpango wa kuanza kutekeleza katika mwaka wa fedha 2025.

*"Kwa Mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imepanga kujenga Ofisi za Wilaya 24 kwa kutumia Mfumo wa Matumizi ya Rasilimali za Ndani (Force account). Ofisi ilifikia uamuzi wa kutumia njia hii ili kupunguza gharama na kuwezesha kujenga ofisi nyingi Zaidi".*

Kikao hicho kililenga kutoa mafunzo ya Sheria,kwa njia ya mfumo wa matumizi ya rasilimali za ndani kwa lengo kupata uelewa wa pamoja.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka alifafanua kuwa, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imedhamiria kwa dhati kutekeleza miradi ya ujenzi katika Mikoa na Wilaya ili kusogeza huduma kwa wananchi ambapo aliongeza kuwa mkakati wa Ofisi ni kuendelea kuanzisha Ofisi mpya na wakati huo huo kuendelea kujenga majengo ya ofisi ili kuwezesha upatikanaji wa mazingira mazuri ya utoaji wa huduma.

*"Tunawategemea sana kwenda kusimamia ujenzi wa Ofisi zetu za wilaya kwa kutumia kiasi cha pesa ambacho kimetengwa. Ni jukumu ambalo tumewapa na kuwaamini sana na pia ni jukumu ambalo litahitaji moyo wa uzalendo sana, tutambue ya kuwa fedha hiyo ni fedha ya Serikali, fedha ya walipa kodi, na tumeamua kutumia njia hii ili tuweze kujenga ofisi nyingi zenye ubora na kwa gharama nafuu"*, alisisitiza Naibu Mkurugenzi Bibiana.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Simon Ntobbi aliwataka washiriki hao kwenda kusimamia kwa weledi mkubwa shughuli za ujenzi wa majengo ya Ofisi za wilaya pasipo udanganyifu wa aina yoyote na kuhakikisha wanasimamia ujenzi huo kama wanavyosimamia mali zao binafsi kwa sababu fedha hizo ni Mali ya Umma.

Wataalamu kutoka Wakala wa Ununuzi wa Umma na Wizara ya Fedha walielimisha washiriki juu ya masuala mfumo wa ujenzi kwa kutumia Mfumo wa Matumizi ya Rasilimali za Ndani ambapo washiriki walipata fursa ya kuuliza maswali mbalimbali.

# Watumishi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Wakumbushwa Kuendelea Kufanya Kazi kwa Ufanisi

*Na Ally Masaninga*



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari akisisitiza jambo wakati wa kikao cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kilichofanyika Jijini Dodoma.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari amewakumbusha watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na ushirikiano ili kuleta matokeo chanya zaidi.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa rai hiyo wakati akizungumza katika kikao na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali kilichofanyika Jijini Dodoma tarehe 18 Agosti, 2025.

***"Niwakumbushe watumishi kuendelea kutekeleza majukumu kwa ufanisi na ushirikiano, tuendelee kuzingatia Weledi na Ubora."*** Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitumia kikao hicho kuwafahamisha rasmi Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa iliyokuwa Divisheni ya Uandishi wa Sheria imekuwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na imeanza kutekeleza majukumu yake kuanzia tarehe 1 Julai, 2025, ambapo ameeleza kuwa lengo la maboresho hayo ni kuongeza tija katika utoaji wa huduma za Uandishi wa Sheria.

*"Msije mkafikiria kuwa Ofisi ya Mwandishi wa Sheria imeondoka moja kwa moja, ni sehemu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kinachofanyika kitaalamu kinaitwa functions separation ili kuongeza tija."* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Vilevile Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi wa Sheria zitaendelea kuimarisha mahusiano ili kuhakikisha kwamba ufanisi unaotarajiwa katika Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria unaonekana.

Akifunga kikao hicho, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno aliwasisitizia Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuisoma na kuielewa Dira 2050 ili waweze kuitekeleza Dira hiyo kwa ufanisi mkubwa.

*"Nawakumbusha watumishi wote kuipitia na kuisoma Dira 2050 na kuielewa vizuri na hata kipindi mnatoa Ushauri wa Kisheria kuhusiana na Dira hii mtoe Ushauri utakaokuwa sahihi katika utekelezaji wa Dira."* Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hatua nyingine, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasisitiza watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushiriki katika mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo yaliyoanishwa katika mpango kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili waweze kuongeza ujuzi na kuwawezesha kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

*"Niwaombe watumishi wa Ofisi hii muendelee kutumia fursa hii ya mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo sisi viongozi wenu tutahakikisha watumishi wote mnapata mafunzo haya ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa ufasaha."* Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Awali, Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole, akitoa wasilisho kuhusiana na uanzishwaji wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria alisema kuwa kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria ni mojawapo ya jitihada za Serikali katika kuendelea kuimarisha na kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sambamba na hilo, Mwandishi Mkuu wa Sheria alisema kuwa kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kutawezesha utekelezaji wa masuala ya Uandishi wa Sheria, Urekebu wa Sheria na Ufasiri wa Sheria kwa uwanda mpana zaidi.

*"Kuanzishwa kwa Ofisi hii kutaongeza na kuwezesha masuala ya uandaaji wa Miswada, Urekebu wa Sheria na Ufasiri wa Sheria kutekelezwa kwa upana wake kwa kuwa tutakuwa na wataalamu wa kutosha."* Alisema Mwandishi Mkuu wa Sheria



Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole akifanya wasilisho kuhusiana na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wakati wa kikao cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kilichofanyika Jijini Dodoma.



Baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakifuatilia mijadala mbalimbali wakati wa kikao cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kilichofanyika Jijini Dodoma.

# Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Awaongoza Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kushiriki Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake

*—— Na Prisca Ulomi ——*




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Watumishi wa Umma, Sekta binafsi na Wananchi wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika Jijini Arusha.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo amewaongoza Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kushiriki Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika Kitaifa katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Jijini Arusha.

Akizungumza mara baada ya sherehe za maadhimisho hayo, Bi. Mtulo aliwahimiza wanawake hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, bidii, uaminifu na weledi katika kila kazi wanazopewa ili kufikia malengo waliyojiwekea kwa wakati.


Bi. Mtulo alisisitiza kuwa upo umuhimu wa wanawake kutokujenga tabia ya kuchagua kazi, akieleza kuwa kufanya hivyo kutawasaidia kujiongezea kipato na kuboresha maisha yao.

Alieleza kuwa hatua madhubuti zinazochukuliwa na wanawake kote duniani zina mchango mkubwa katika kufanikisha lengo la usawa wa kijinsia la 50 kwa 50.

Aidha, aliwataka wanawake kushikilia nafasi zao kwa weledi ili kusaidia juhudi za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuliletea taifa maendeleo.

Maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa katika jiji la Arusha yalihudhuriwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo katika hotuba yake, Rais Samia aliwahimiza wanawake kote nchini kuendelea kujituma na kufanya kazi kwa bidii ili kujikwamua kiuchumi kwa kuwa Serikali imeweka mazingira bora ya uwekezaji ili kuwawezesha wanawake, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mikopo nafuu inayowawezesha kukopa na kulipa kidogo kidogo baada ya kupata faida kubwa.

Ushiriki wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika maadhimisho haya unaonyesha dhamira ya taasisi katika kuendeleza juhudi za Serikali za kuhakikisha usawa wa kijinsia na maendeleo ya wanawake katika sekta mbalimbali nchini.



Nalbu Wakili Mkuu wa Serikall, Bi Alice Mtolo (aliyeketi katikati kushoto) akimsikiliza Rais wa Jemhuri ya Muungario wa Tanzania, Mhe. Dikl. Samia Suluhu Hassan akihutubia wananchi wakati wa Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika JijiniArusha.



Baadhi ya Watumishi Wanawake kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakipita mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzanie, Mhe. Dkt. Sarnia Suluhu Hassan wakati wa Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika Jijini Arusha.

# "Uchunguzi wa Makosa ya Kifedha ni Nguzo Muhimu Sana Katika Mapambano Dhidi ya Uhalifu wa Kiuchumi". Mhe. Rose Ibrahim

*Na Rebecca Kwandu*



Jaji Mfawidhi wa Mahamaka Kuu ya Tanzania Kanda ya Morogoro Mhe. Rose Ibrahim wakati akifungua Mafunzo kwa Wadau wa Haki Jinai kuhusiana na Uchunguzi wa Makosa ya Kifedha na Uchunguzi wa Kisayansi yaliyofanyika Mkoani Morogoro.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Morogoro Mhe. Rose Ibrahim amesema uchunguzi wa Makosa ya kifedha ni nguzo muhimu sana katika mapambano dhidi ya uhalifu wa kiuchumi kwani Wahalifu wengi wa makosa hayo wamekuwa wakiibua mbinu mbalimbali za kidigitali ikiwemo kuunda mitandao tata isiyofikika kirahisi na mbinu za kawaida.

*"Kwenye makosa ya kifedha Wahalifu wengi huwa wanatumia mbinu za kiteknolojia kutenda au kuwezesha utendekaji wa makosa hayo, hivyo Wapelelezi na Waendesha Mashtaka lazima wawe na ujuzi wa kutosha kufaa kukusanya ushahidi wa kielektoniki na kufuata Sheria zilizowekwa ili kusimama vyema bila kupoteza ushahidi",*

Mhe. Jaji aliyasema hayo wakati akifungua Mafunzo yaliyofanyika tarehe 25 na 26 Aprili, 2025 Mkoani Morogoro, kwa wadau wa Haki Jinai kuhusiana na Uchunguzi wa Makosa ya Kifedha na Uchunguzi wa Kisayansi

Jaji Mfawidhi alisema ni muhimu mafunzo hayo kufanyika kwa kila mwaka ili kuweka utaratibu wa kuwa na mafunzo endelevu ya kubaini mbinu zinavyobadilika kila kukicha kwani itasaidia kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu kwa mambo au mbinu na changamoto ambazo wengine wanakutana nazo na namna bora ya kukabiliana nazo.

Katika hatua nyingine, Mhe. Jaji Rose Ibrahim alisisitiza juu ya umuhimu mkubwa wa Ushahidi wa Kisayansi katika utendaji wa haki ambapo kwa sasa Sayansi na Teknolojia vimeshika hatamu.

*"Ni lazima tuwe na maarifa na mbinu za kutosha za kiupelelezi na ukusanyaji ushahidi unaojibu makosa ya kifedha ili kuisaidia mahakama kutoa maamuzi yaliyosahihi kwa upande wa mashtaka na kuweza kutaifisha mali zinazotokana na makosa husika."* Alifafanua Mhe. Jaji Rose.

Sambamba na hilo, aliwataka Waendesha Mashtaka na Wapelelezi kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuwawezesha kupata ushahidi wa uhakika na uliokamilika.

Aidha, alisema Mashtaka bila ufuatiliaji wa mali ni ushahidi nusu, ambao bado haujakamilika. Uhalifu wa kifedha siyo tu kuwafikisha wahusika Mahakamani bali ni kuhusu Urejeshaji wa mali, Uwajibikaji na kutoa fundisho kwa wengine.

Mali yoyote au fedha inayoporwa kutoka kwa umma au wananchi inapaswa kurejeshwa na kila mhalifu hana budi kuadhibiwa pamoja na kupokonywa faida ya uhalifu huo.




# "Sisi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tunaamini Nyinyi Wahariri ni Askari wa Kalamu" - Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

*Na Ally Masaninga*

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno amesema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaamini kuwa Wahariri wa Vyombo vya Habari ni Askari wa Kalamu kwakuwa wana uwezo wa Kuelimisha, Kulinda na Kusimamia masuala mbalimbali yanayogusa Jamii ikiwemo misingi ya Sheria na Utawala Bora.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyasema hayo wakati wa Ufunguzi wa Kikao cha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini tarehe 11 Septemba, 2025 Jijini Dodoma.

Akizungumza katika ufunguzi wa kikao hicho, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza kuwa Serikali inatambua mchango mkubwa wa Vyombo vya Habari katika kujenga Utawala Bora na Uwazi ambapo alisema kuwa Vyombo vya Habari ni daraja muhimu la kuunganisha Serikali na wananchi, na ndio maana ni muhimu sana kwa wahariri kuwa na uelewa wa kutosha wa masuala ya kisheria ili waweze kuripoti kwa usahihi na bila upotoshaji.

*"Sisi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunaamini nyinyi Wahariri wa Vyombo vya Habari ni Askari wa Kalamu kama tulivyo sisi Mawakili wa Serikali, kwakuwa mna jukumu muhimu la kulinda na kusimamia misingi ya Utawala Bora kwa kutoa taarifa sahihi kwa wananchi."* Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hatua nyingine, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kupitia kikao hicho Wahariri watapata uelewa wa kutosha wa majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia mada zitakazolenga kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kisheria hususan katika maeneo ya Ushauri wa Kisheria, Uandishi wa Sheria pamoja na Majadiliano na Upekuzi wa Mikataba.

*"Ni matarajio yetu kuwa, mtakuwa huru kutoa maoni yenu yatakayorahisisha uelimishaji katika kuripoti masuala ya kisheria na hatimaye kusaidia kuondoa baadhi ya upotoshaji unaoweza kujitokeza katika kuripoti taarifa za kisheria"*. Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kufanya maboresho mbalimbali ya Sheria ili ziweze kuakisi Malengo ya Utekelezaji wa Dira 2050 ambapo alieleza kuwa maboresho hayo yanafanyika

kwa lengo la kuendana na mabadiliko ya Kijamii na Kiuchumi kufikia Dira 2050.

*"Kwa upande wetu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunahakikisha maelekezo ya Mhe. Rais yanatekelezwa kwa ufanisi na weledi mkubwa kwa kuhakikisha tunaoanisha Sheria tulizonazo na kule tunakotaka kwenda ili ziakisi malengo ya Dira 2050."* Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Awali, akizungumza kwa Niaba ya Msemaji Mkuu wa Serikali, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) Bw. Rodney Thadeus aliwataka Wahariri wa Vyombo vya Habari kukitumia kikao kujifunza masuala mbalimbali ya kisheria yatakayoelezwa kwenye kikao hicho ili waweze kutoa taarifa zilizo sahihi na zenye maslahi kwa taifa.

*"Ndugu zangu Wahariri wa Habari tuendelee kusimamia misingi na weledi ya Uandishi wa Habari ili tuweze kuripoti taarifa kwa usahihi na weledi mkubwa".* Alisema Bw. Rodney

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya kikao na Wahariri wa Vyombo vya Habari kwa siku mbili ambapo kikao hicho kilianza tarehe 11 hadi 12 Septemba, 2025.




Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) Bw. Rodney Thadeus akizungumza kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Serikali katika kikao cha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wahariri wa Vyombo vya Habari kilichofanyika Jijini Dodoma.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno (katikati walioketi), akiwa katika picha ya pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole (wa kwanza kushoto walioketi), Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) Bw. Rodney Thadeus (wa pili kushoto walioketi), Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Bw. Bakari Machumu (wa pili kulia walioketi) na Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini.

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yasogeza Huduma Karibu na Wananchi

*Na Prisca Ulomi*



Picha ya muonekano wa Jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali linaloendelea kujengwa katika Mji wa Serikali - Mtumba Jijini Dodoma.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekasimiwa dhamana ya kusimamia, kuratibu na kuendeshamashauri ya madai na usuluhishindani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake. Kwa kuzingatia umuhimu wa dhamana hiyo, Serikali imeipatia eneo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mtumba-Mji wa Serikali Dodoma ili iweze kuwa na Ofisi ya kudumu na Makao Makuu ya Ofisi hiyo kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa Serikali na taasisi zake na kusogeza huduma karibu na wadau na wananchi.

Ili kuhakikisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatimiza azma ya Serikali kuhamia Dodoma, Ofisi inaendelea na ujenzi wa Jengo katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Ujenzi huo ni wa jengo la ghorofa nne (04) lenye sakafu sita (06).

Ujenzi unafanyika kwenye eneo la ukubwa wa mita za mraba 17,342 na unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni ishirini na sita, milioni mia saba na arobaini, laki tatu na elfu sita, mia moja kumi na moja na senti sabini na tisa (26,740,306,111.79).

Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni ishirini na sita, milioni mia mbili arobaini na mbili, laki tisa ishirini na sita, elfu sitini na moja na senti sabini na mbili (26,242,926,061.72) ni kwa ajii ya mkandarasi SUMA JKT Construction Ltd na kiasi cha shilingi milioni mia nne tisini na saba, laki tatu themanini na hamsini elfu (497,380,050.00) zililipwa kwa ajili ya huduma za ushauri elekezi kwa Wakala wa Majengo Tanzania - TBA.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2025; Ofisi imepokea na kulipa kiasi cha shilingi bilioni kumi na saba, milioni mia tatu sabini na nane, sitini na nne elfu na mia mbili hamsini na saba na senti thelathini nne (17,378,064,257.34) ambapo kiasi cha shilingi bilioni kumi na mbili (12,000,000,000.00) ni kwa ajili ya Mkandarasi SUMA JKT Construction Ltd na kiasi cha shilingi milioni mia mbili tisini na nane, laki sita sitini na nane, thelathini elfu na senti sifuri (298,668,030.00) ni kwa ajili ya Mshauri elekezi Wakala wa Majengo Tanzania - TBA. Aidha, hadi kufikia mwezi Julai, 2025 Ujenzi umefikia asilimia 65.

# Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Washiriki Kwenye Maadhimisho ya Mei Mosi, 2025 Mkoani Singida

*Na Rebecca Kwandu*

Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kutoka Makao Makuu Jijini Dodoma, Mkoa wa Singida, Dodoma na Manyara pamoja na wawakilishi wa TUGHE kutoka baadhi ya mikoa wakiongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu, wameungana na Wafanyakazi wengine nchini kuadhimisha siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) ambapo Kitaifa imeadhimishwa tarehe 01 Mei, 2025 kwenye viwanja vya Bombadia Mkoani Singida.

Mgeni rasmi kwenye maadhimisho haya yaliyoandaliwa na Shirikisho la vyama 13 vya Wafanyakazi (TUCTA) alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema kuwa katika kuzidi kuleta ustawi kwa wafanyakazi nchini, Serikali imefanya maamuzi ya kupandisha kima cha chini cha mshahara kwa watumishi wa umma kwa asilimia 35.1.

*"Ninayo furaha ya kuwatangazia kwamba, katika kuzidi kuleta ustawi kwa wafanyakazi, mwaka huu, Serikali itaongeza kima cha chini cha mshahara kwa watumishi wa umma kwa asilimia 35.1, nyongeza hii itakayoanza kutumika mwezi Julai, 2025 itaongeza mshahara wa kima cha chini kutoka Shilingi 370,000/= hadi Shilingi 500,000/=. Ngazi nyingine za mshahara nazo zitapanda kwa viwango tofauti tofauti kulingana na uwezo wa kibajeti."* Alifafanua Mhe. Rais.

Aidha, maadhimisho hayo yalibeba kauli mbiu isemayo *"Uchaguzi Mkuu 2025, Utuletee viongozi wanaojali haki na Maslahi ya Wafanyakazi, Sote tushiriki."*



*Kutoka Bungeni*

# Bunge Lapitisha Miswada Miwili ya Marekebisho ya Sheria

*Na Leila Muhaji*



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari akiwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024, Bungeni Jijini Dodoma.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha Miswada Miwili ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali ya mwaka 2024, tarehe 29 Januari, 2025 katika kikao cha pili cha Mkutano wa kumi na nane wa Bunge. Miswada iliyopitishwa ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2024 (The written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill 2024, na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimball (Na. 4) wa Mwaka 2024 (The written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill 2024 No. 3) Bill 2024.

Akizungumza wakati wa kuwasilisha Miswada hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari alisema kuwa Miswada hiyo inakusudia kufanya marekebisho katika jumla ya Sheria kumi na mbili.

*"Malengo ya marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya sheria husika na kuzifanya sheria hizi ziendane na wakati na kuleta tija kwa wananchi".* Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alizitaja Sheria zilizofanyiwa marekebisho ni pamoja na Sheria ya Mawakili Sura ya 341, Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu Sura ya 3, Sheria ya Huduma za Jamii Sura ya 291, Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo Sura ya 132, Sheria ya Madini Sura ya 123 na Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298.

> ***"Malengo ya marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya sheria husika na kuzifanya sheria hizi ziendane na wakati na kuleta tija kwa wananchi"***

Mhe. Johari aliendelea kuzitaja Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423, Sheria ya Vyama vya Ushirika Sura ya 211, Sheria ya Tasnia ya Pamba Sura ya 201, Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi Sura ya 386, Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Sura ya 435, Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura ya 418.

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema marekebisho hayo yatasaidia kutatua changamoto na mapungufu mbalimbali yaliyokuwepo katika Sheria hizo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Joseph Mhagama alifurahishwa na hatua za Bunge kupitisha Miswada hiyo ambayo inakwenda kuleta maboresho katika utekelezaji wa Sheria zilizorekebishwa hivyo kupelekea mabadiliko ya Kiuchumi na Kijamii kwa watanzania.

*"Nalipongeza Bunge kwa kupitisha Miswada hii miwili ambayo inakwenda kuboresha na kuleta tija katika Sekta mbalimbali".* Alisema Dkt. Mhagama.

Baada ya Miswada hiyo kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipelekwa kwa Mhe. Rais kwa ajili ya kusainiwa na kuwa Sheria kamili.

# "Toeni Elimu ya Sheria za Uchaguzi kwa Wananchi"- Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

*—— Na Ally Masaninga ——*

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno, amekutana na kufanya mazungumzo na Ujumbe kutoka Kampuni ya The Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya The Guardian na Nipashe, katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma, tarehe 26 Juni, 2025.

Mazungumzo hayo yalilenga kuimarisha mahusiano kati ya taasisi za kiserikali na vyombo vya habari pamoja na kujadiliana juu ya Taasisi hizo zinavyoweza kushirikiana katika kuwahabarisha wananchi majukumu na mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa katika Sekta ya Sheria.

Akizungumza katika kikao hicho, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa ni muhimu kwa vyombo vya habari kutoa elimu ya Sheria ya Uchaguzi kwa wananchi ili waweze kuielewa.

*"Niwaombe muendelee kutoa elimu ya sheria mbalimbali na katika kipindi hiki tulichopo toeni elimu ya kutosha kuhusu Sheria za Uchaguzi ili wananchi waweze kuielewa."* Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza kuwa Ofisi yake iko tayari muda wowote kushirikiana na vyombo vya habari ili kuweza kutoa taarifa sahihi kwa wananchi, pia alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatambua mchango mkubwa wa vyombo vya habari katika kukuza demokrasia, kutoa elimu kwa umma na kushirikiana na taasisi za umma katika kuhimiza utawala bora.

*"Tunatambua nafasi ya vyombo vya habari katika kutoa elimu kwa wananchi, Ofisi yetu iko wazi muda wote kushirikiana nanyi katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi kupitia vyombo vya habari".* Alieleza Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wake, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa The Guardian Limited Bw. Jackson Paul ameishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mapokezi mazuri waliyoyapata na ziara yao imekuwa na mafanikio makubwa kwakuwa wamejifunza mambo mengi ya kisheria huku akiahidi wataendeleza ushirikiano huo kwa kuuhabarisha umma juu ya masuala mbalimbali ya kisheria yanayotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*"Tunawashukuru sana kwa kutupokea, kipekee nikushukuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutenga muda wako na kuzungumza nasi, tumejifunza mambo mengi ambayo tutaenda kuyafanyia kazi."* Alisema Bw. Jackson

Ujumbe kutoka Kampuni ya The Guardian Limited uliotembelea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali uliongozwa na Naibu Mkurugenzi Mtendaji Bw. Jackson Paul, Mhariri wa Habari Bi. Salome Kitomari, Mkuu wa Masoko Kanda ya Kati Bw. Raymond Mushi, Msimamizi wa Mkoa wa Dodoma Bi. Linda Samwel, Afisa Masoko Bi. Sekela Kilembe na Mwandishi wa Gazeti la Nipashe Bw. Peter Mkwavila.

Aidha, katika hicho kilichoongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno kilihudhuriwa pia na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Leila Muhaji na Wakili wa Serikali Bw. Hassan Nkya.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno akizungumza na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa The Guardian Limited Bw. Jackson Paul (kushoto) na Mhariri wa Gazeti la Nipashe Bi. Salome Kitomari wakati ujumbe huo kutoka Kampuni ya The Guardian ulipotembelea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mtumba, Jijini Dodoma.

# Kamati ya Bunge Yapongeza Serikali Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Temeke

*Na Rebecca Kwandu*

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imeipongeza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Mikoa na Wilaya na kueleza kuwa hatua hiyo itasaidia kusogeza huduma kwa wananchi pamoja na kuweka mazingira bora ya utoaji wa huduma za mashtaka ya Jinai nchini jambo litakalosaidia upatikanaji wa haki kwa wananchi na kulinda amani na usalama ambayo ni dhamira ya Serikali na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza mara baada ya kamati hiyo kukagua maendeleo ya miradi ya ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Mikoa ya Kimashtaka Temeke na Kinondoni jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Bunge Mhe. Dkt. Joseph Mhagama alieleza kuwa Kamati hiyo imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Ofisi hizo za Mikoa ya Kimashtaka Temeke na Kinondoni ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2025

Akizungumza katika ziara ya kukagua maendeleo ya miradi hiyo, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, aliipongeza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa maono na utashi wa kutekeleza miradi hiyo ya kimkakati na kueleza imetokana na uongozi bora wa viongozi waliopo.

*"Mimi ni Wakili hadi sasa, nimefanya kazi ya Uwakili kwa miaka zaidi ya 30 na nimefanya kazi na Wakurugenzi wa Mashtaka wengi, lakini nikupongeze Mkurugenzi wa Mashtaka Mwakitalu kwa mageuzi haya makubwa ambayo yanahitaji utashi mkubwa, uadilifu na kujitoa."* Alisema Waziri Ndumbaro.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu alimshukuru Mhe. Rais, Kamati ya Bunge na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuiwezesha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kufanya mageuzi haya muhimu na kueleza kwamba miradi inayoendelea kutekelezwa ni matunda ya Kamati hiyo.

Mkurugenzi Mwakitalu alisema kuwa, miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni sehemu ya miradi inayoendelea kutekelezwa katika mikoa mingine ipo katika hatua mbalimbali na kwamba kuanzia mwaka 2025 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pia imeanza kutekeleza miradi ya ujenzi ya Ofisi za Mashtaka za Wilaya ambapo hadi sasa ujenzi umeanza katika wilaya 24.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe. Sixtus Mapunda kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila alitoa pongezi kwa kutekelezwa kwa miradi hiyo ya ujenzi katika wilaya hizo na kuongeza kwamba miradi hiyo itakua na tija kwa wananchi.

Aidha, Waziri wa Afya Nchini Mhe. Jenister Mhagama ambaye pia ni mjumbe wa kamati hiyo, alisema kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwezesha utekelezaji wa miradi hiyo ambayo itachochea upatikanaji wa haki kwa wananchi ambapo pia aliipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa usimamizi mzuri wa taasisi zake katika utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na serikali.

Sambamba na hilo, alitoa rai kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuendelea kusimamia miradi hiyo ili ikamilike kwa asilimia 100 kwa ufanisi ndani ya muda uliopangwa kulingana na mkataba uliopo. Ziara ya Kamati ya Bunge Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilifanyika tarehe 12 Machi, 2025.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria wakiwa wameambatana na viongozi na watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakikagua jengo la Ofisi hiyo mkoa wa kimashtaka Temeke.




**Matukio katika Picha:**
**Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akikabidhi Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la mwaka 2023 kwa Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. George Masaju.**










# Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu Toleo la Mwaka 2023



# Sauti ya Sheria

Toleo Na. 1 — Julai - Disemba 2025

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka
Chuo Kikuu cha Dodoma
Jengo la Taaluma
Na.2 S.L.P 1733, Dodoma
dpp@nps.go.tz I www.nps.go.tz
+255 26 2963634

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mji wa Serikali - Mtumba
S.L.P 630, Dodoma
Tanzania info@oag.go.tz
www.oag.go.tz
+255 26 2961941

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali
10 Barabara ya Kivukoni
S.L.P 71554,
11101 Dar es Salaam
Info@osg.go.tz I www.osg.go.tz
+255 22 2127384

## Mafanikio katika Sekta ya Sheria, Usimamizi wa Mikataba na Uendeshaji Mashauri ya Madai na Jinai

oagtanzania | oag_tz | oagtanzania | Mwanasheria Mkuu TV

omashtaka | Ofisi ya_taifa ya_mashtaka | Mashtaka TV

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | osgtanzania | osgtanzania | Wakili Mkuu TV